MID WEEK JACKPOT!
TZS. 560,305,280
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.co.tz
PIGA *150*87#



**Polisi** Kanda Maalum ya Dar wawasilisha hoja Tume ya Hakijinai

UKURASA 2




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Aprili 24, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581290

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



RIPOTI YA UCHUNGUZI

USALAMA HIFADHI ZA TAIFA...

# Kampuni yachimba madini hifadhini

• **Watendaji** serikalini wako njiapanda... *Endelea ukurasa 4*


Waziri wa Madini, Dotto Biteko.



Licence ML 05/92

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF MINERALS
MINING COMMISSION

RENEWAL OF MINING LICENCE No. ML 05/92

I, Prof. Shukrani E. Manya, **EXECUTIVE SECRETARY**, pursuant to the powers conferred up on me under section 53 of Mining Act, Cap.123 hereby renew Mining Licence No. **ML 05/92** granted to M/S **Seasalt Limited** of **P.O.Box 9474, Dar es Salaam, Tanzania** located at **Sadani** area in **Bagamoyo** District for a period of **ten** (10) years effective from **18/05/2020.**

This License is being renewed subject to the Mining Act, Cap.123 and terms and conditions of Mining licence No. **ML 05/92.**

**IN WITNESS WHEREOF,** this renewal is signed

this 12th day of MAY 2020

Prof. Shukrani E. Manya
EXECUTIVE SECRETARY

## Waziri Mwigulu ataja mbinu za kukabili ushoga



UKURASA 3

# JKCI ilivyookoa maisha ya kijana aliyekunywa 'energy'




• **Mishipa** ya moyo wake iliziba ghafla... *Endelea ukurasa 2*





Kampuni ya the Guardian Limited, Wachapishaji wa Magazeti ya the Guardian na Nipashe, inawakaribisha wadau wote wa maendeleo kutoa salaam za pongezi wakati tunaadhimisha miaka 59 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Toleo hili litachapishwa tarehe 26 Aprili, 2023 kwenye Magazeti ya Guardian na Nipashe.

The Guardian Nipashe

Kwa mawasiliano zaidi,
Tupigie +255 677 020 701

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com

# JKCI ilivyookoa maisha ya kijana aliyekunywa 'energy'

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) imebainisha namna ilivyookoa maisha ya kijana mwenye umri wa miaka 28, mtanzania aliyefikishwa katika taasisi hiyo kwa matibabu ya dharura.

Imefafanua kuwa kijana huyo ilimpokea akiwa anasumbuliwa na maumivu makali ya kifua upande wa kushoto, uliko moyo, kutokana na kunywa kinywaji cha kuongeza nguvu, maarufu 'energy'.

Kwa mujibu wa Bingwa wa Magonjwa ya Moyo na Mkuu wa Kitengo cha Utafiti na Mafunzo wa JKCI, Dk. Pedro Pallangyo, uchunguzi wa awali ulibaini kijana huyo hakuwa na magonjwa hatarishi yasiyoambukiza kama ya moyo, yanayosababishwa na vilevi, uvutaji sigara na uzito mkubwa.

Bingwa huyo alibainisha hayo jana alipofafanua kwa waandishi wa habari, akisema kesi kama hiyo huwa ni nadra kutokea, hivyo taasisi ikaamua kufanya uchunguzi kuanzia mwishoni mwa mwezi Februari hadi Machi mwaka huu, ili kupata undani wa tatizo la kijana huyo.

Alisema kuwa uchunguzi ulihusisha historia ya familia na vifo vya ghafla, ikabainika hakukuwa na historia hiyo, badala yake uchunguzi ulibaini sababu kuu ni unywaji wa vinywaji vya kuongeza nguvu. "Baada ya uchunguzi tulibaini mgonjwa huyo ni mtumiaji wa 'energy drinks' (vinywaji vya kuongeza) ambavyo ni vinywaji," alisema bingwa huyo wa moyo na kuvitaja ni vinywaji vinavyoongeza nishati na nguvu mwilini.

Mtaalamu huyo aliendelea na ufafanuzi wake akitamka: "Kwa siku sita alikuwa amekunywa makopo matano na kila kopo lina ujazo wa milimita 250.

"Kwa ujumla alikuwa amekunywa lita moja na robo, ndani ya saa nne, na baada ya muda huo akimalizia kopo la mwisho ndipo alipopata maumivu makali ya upande wa kushoto, akaja kwetu (JKCI) baada ya awali kutumia tiba nyingine kutuliza maumivu kugoma."

Bingwa huyo alibainisha kwamba, mgonjwa baada ya kufikishwa katika taasisi hiyo na kufanyiwa vipimo vya damu vilikuwa sawa, isipokuwa homoni mbili za moyo zilikuwa zimepanda, akifafanua sababu ya homoni kupanda mara nyingi husababishwa na mishipa ya moyo kuziba.

Alisema vipimo vya moyo kwa mgonjwa huyo vinavyoitwa ECHO na ECG, vyote vilionyesha dalili za mishipa ya moyo upande wa kushoto kuziba, hivyo alianzishiwa matibabu ya dharura.

Alisema kuwa katika matibabu hayo, mgonjwa akiwa maabara ya moyo, iligundulika mshipa wake wa kushoto umeziba kwa asilimia 100 na kwamba hali hiyo ingendelea saa kadhaa, ingesababisha misuli ya moyo kufa na hatimaye kifo cha ghafla.

"Huyu mgonjwa tulifanikiwa kuzibua mishipa yake. Mara nyingi mishipa ya namna hii huwakumba watu wazima hasa wenye kisukari, presha na magonjwa mengine baada ya mafuta kutanda kwenye mishipa. Ila huyu kijana kilichoziba ni donge la damu, liliganda," alifafanua bingwa huyo.

Alisema kuwa baada ya kupatiwa matibabu, mgonjwa huyo alirejeshwa wodini, huku akiwa amewekewa mrija kwenye eneo lililoziba na kutakiwa kuanza kutumia dawa kila siku, maisha yake yote.

"Lazima tujifunze na tuelimshe jamii kuhusu wimbi kubwa la unywaji vinywaji hivi hasa kwa vijana. Wengi hawafahamu madhara ambayo yanaweza kusababisha vifo vya ghafla," alionya Dk. Pedro.



Mke wa Rais wa Zanzibar ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), Mama Mariam Mwinyi akigawa zawadi kwa watoto katika kijiji cha SOS Mombasa, Wilaya ya Magharibi "B", Mkoa wa Mjini Magharibi alipofanya ziara maalum ya kutembelea vituo vya watoto katika kusherehekea Sikukuu ya Eid el fitr juzi. **PICHA: IKULU**

# Hatima mchakato Katiba mpya kujulikana wiki hii

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUTANO wa 11 wa Bunge la 12 ambao ni mahususi kwa bajeti ya serikali 2023/24, leo unaingia juma la nne ambalo pamoja na mambo mengine, hatima ya mchakato wa Katiba mpya inatarajiwa kujulikana.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Bunge, wiki hii wabunge watajadili makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Wizara ya Madini na Wizara ya Katiba na Sheria.

Miongoni mwa mambo yanayotarajiwa kupatiwa ufafanuzi na Wizara ya Katiba na Sheria ni kukwamua mchakato Katiba mpya pamoja na marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa na ya uchaguzi.

Hivi karibuni, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Wizara hiyo jijini hapa, alisema mchakato wa Katiba mpya unatarajiwa kuanza kufanyiwa kazi baada ya kupitishwa kwa bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2023/24.

"Mchakato wa Katiba mpya ni agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, hivyo ili kufanikiwa, mchakato wake unahitaji rasilimali fedha nyingi na wajumbe wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi mtambue mna jukumu hilo la kupitia mapendekezo ya bajeti ya mwaka huu 2023/24 kufanikisha mambo hayo makubwa ya kitaifa," alisema.

Dk. Ndumbaro alisema hitaji la Katiba mpya ni la watanzania, hivyo wizara yake inatakiwa kujipanga kuhakikisha inakamilisha mchakato huo kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwakani na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

"Marekebisho ya sheria za uchaguzi huo yanahitajika pamoja na Sheria ya Tume ya Uchaguzi, hivyo wizara yetu inahitaji rasilimali fedha kupitishwa ili kukamilisha michakato hiyo haraka," alisema.

# Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam wawasilisha hoja Tume ya Hakijinai

**Na Christina Mwakangale**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limewasilisha kwa Tume ya Kuangalia Namna ya Kuboresha Mifumo ya Hakijinai, maoni yake ya kuboresha mwenendo wa kazi wa jeshi hilo, likivitaja vikwazo vya majukumu ya kazi kisheria.

Kamanda wa kanda hiyo, Jumanne Muliro alibainisha hayo mwishoni mwa wiki baada ya tume hiyo inayoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu Othman Chande, kutembelea kanda hiyo.

Muliro alisema zipo changamoto nyingi ambazo zinasababisha mkwamo wa utendaji kazi kisheria, akisisitiza ana imani maeneo waliyowasilisha kwa tume yanayohusu kanda hiyo, yatafanyiwa kazi.

"Kuna maeneo mengi sana ambayo tumewapitisha yakiwamo ya kisheria, rasilimali watu, vifaa, migongano ya kisheria na utekelezaji wake hasa ngazi ya chini.

"Tumewaonyesha changamoto za kisheria na za kiutendaji. Tuwape fursa waziangalie kisha waende kwenye mchakato," alisema Kamanda Muliro.

Wakati wa ziara ya tume hiyo juzi, miongoni mwa maeneo yaliyotajwa kuwa na changamoto na kuathiri utendaji kazi mifumo na taasisi zingine ni pamoja na kuchelewa kwa upelelezi kunakosababisha Jeshi la Magereza kuwa na msongamano wa mahabusu gerezani.

Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Magereza ambaye pia ni Wakili wa Serikali, Theophil Rwiukya, akisoma taarifa mbele ya tume hiyo ilipotembelea Gereza la Ukonga jijini, alisema kubadilishwa maelezo polisi, ubambikwaji kesi na kutokamilishwa upelelezi kwa wakati ni changamoto kwa utendaji wao.

Alisema changamoto hizo ambazo huanzia Jeshi la Polisi, ikiwamo mahojiano kuchukua muda mrefu, zinasababisha magereza kuwa na msongamano zaidi ya uwezo.

Pia aliwataja wahamiaji haramu kuwa sehemu ya vyanzo vya msongamano wa mahabusu katika magereza yao.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alifanya ukaguzi mahususi kuhusu utolewaji wa hakijinai nchini, akibaini kuwapo uhaba wa askari polisi, majaji na mahakimu, maofisa wapelelezi na mawakili wa serikali.

CAG Charles Kichere pia alibaini ucheweshaji wa upelelezi wa mashauri, msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani na kutokutolewa mafunzo na semina elekezi kwa watendaji wa Mahakama.

HABARI KITAIFA

# Mwigulu ataja mbinu za kuudhibiti ushoga

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (pichani kulia), amesema ili kukabiliana na vitendo vya ushoga na ulawiti nchini, mbali na hatua za kisheria zinazochukuliwa kwa wahusika, kuna haja kuweka mkazo katika maadili.

Akizungumza juzi wakati wa Baraza la Eid lililofanyika Kijiji cha Iteme, Kata ya Mtoa wilayani Iramba mkoani Singida, waziri huyo alisema wazazi na viongozi wa dini wanalo jukumu la kuweka mkazo katika kulea vijana katika misingi impendezayo Mungu na wao wakiishika, hawatoiacha na wala hawatopitiwa na wimbi la ushoga.

"Tutakata matawi lakini kama shina na mizizi ipo, matawi yatakuwa yanachipuka tu. Tuchimbue mizizi tuondoe na shina na msingi wake upo kwenye kuwekeza kwenye maadili.

"Tunapolegalega na kumwacha Mungu, tukifungua milango na madirisha vitu vya ajabu vitapata mwanya lakini tukifunga havitopata nafasi hiyo," alisema.

Dk. Mwigulu, akizungumzia suala la uchumi, alisema pamoja na dunia kupitia kwenye misukosuko ya kiuchumi na majanga, Tanzania haijayumba kutokana na serikali kujipanga vizuri.

"Hakuna siku taifa lilisimama kwenye mitikisiko ya kidunia, siku zote taifa limeendelea, hakuna siku watoto wameshindwa kwenda shuleni, hakuna siku watu wamepata shida ya kuogopa usalama wa maisha yao bali wameendelea na shughuli zao," alisema.

Waziri huyo pia alisema hakuna miradi ya maendeleo iliyokwama - iwe midogo au mikubwa na hayo yote yanafanyika kutokana na uimara wa serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, hivyo wananchi wa dini zote waendelee kumwombea.

"Mafanikio ambayo Tanzania inayo hadi nchi nyingine za Afrika zinashangaa na kujiuliza nchi zao zimekosea nini, mambo haya ukiyaona yamekuwa mepesi si kwamba ni mepesi, ni vile mzigo mzito ukibebwa na mwenye nguvu huanza kuonekana mwepesi," alisema.

Dk. Mwigulu alisema zipo nchi nyingine Afrika ambazo zinafanana na Tanzania ambazo zimepata misukosuko zimefikia hatua hata ya kushindwa kulipa mishahara ya watumishi wake lakini Tanzania haijayumba, Inazidi kusonga mbele.

Sheikh wa Mkoa wa Singida, Issa Nassoro, aliishukru serikali kwa kuwa wakati wa mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani bei za vyakula na nguo hazikupanda na hakukuwa na mfumuko wa bei.

Sheikh Nassoro aliiomba serikali kutoteteleka katika msimamo wake kuhusu suala la ushoga na kusifu hatua zilizoanza kuchukuliwa dhidi ya watu wanaojihusisha na vitendo hivyo.

"Ninaipongeza serikali kutokana na hatua zilizoanza kuchukuliwa kupitia mahakama kwa kuanza kuwahukumu baadhi ya watu wanaojihusisha masuala ya ulawiti na ushoga na hatua hizi zisiishie kwa mashoga tu, bali pia ziende kwa makundi mengine yote yanayojihusisha na mapenzi ya jinsia moja," alisema.



# Ofisa Mtendaji Kata kizimbani mashtaka ubadhirifu wa saruji

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

OFISA Mtendaji wa Kata ya Bulela, John Shatta (35) amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Geita kwa mashataka ya ufujaji na ubadhirifu wa mifuko 20 ya saruji, mali ya Halmashauri ya Mji wa Geita.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani mbele ya Hakimu wa Mahakama hiyo, Johari Kijuile na aliposomewa shtaka lake, alikana kuhusika na kosa hilo na yuko nje kwa dhamana ya mdhamini mmoja na kuweka bondi mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milion 15.

Upande wa mashtaka ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita Ruth Ndetto ambaye alidai mahakamani kuwa upelelezi wa kesi hiyo ya uhujumu uchumi Na. 1/2023 umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Kijuile alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Mei 4 mwaka huu kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa TAKUKURU Mkoa wa Geita, Ndetto, alidai mahakamani kuwa kati ya Novemba 1 mwaka 2022 na Febuari 6 mwaka 2023, Mtaa wa Mwatulole, Mkoa Geita, mshtakiwa alichukua mifuko 20 ya saruji, mali ya Halmashauri ya Mji wa Geita iliyokuwa chini ya uangalizi wake na akaitumia kwa matumizi yake binafsi.

Awali Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Geita, Leonidas Felix, alidai nje ya mahakama kuwa mali hiyo imeshakamatwa na inaendelea kushikiliwa na TAKUKURU.

Felix aliwataka wananchi wa Mkoa wa Geita kuendelea kushirikiana na TAKUKURU katika kuwafichuwa watu wanaojihusisha na ubadhirifu wa mali ya umma ili taifa liwe na maendeleo.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI YA UZALISHAJI NA USAFIRISHAJI WA VIPENGEE VYA ZEGE (PRECAST CONCRETE ELEMENTS)**

**KUMB: ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0119**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwa Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

BESIX Ballast Nedam (BBN) Limited, inayotekeleza Huduma za awali za ujenzi wa Gati na kituo cha kupakilia mafuta ghafi katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa:

**- Uzalishaji na usafirishaji wa vipengee vya zege kwa ajili ya Mihili ya Gati**

**MAELEZO MAFUPI YA UPEO WA VIFAA / HUDUMA:**
- Aina ya zege ni C40/50 XS3.
- Aina ya saruji ni maalum. CEM III/B au CEM II/BV.
- Vipengee vya zege vitawasilishwa kwenye eneo la mradi tarehe 1 Oktoba 2023.
- Uzito wa vipengee utatofautiana kati ya tani 5 hadi tani 63.
- Usafirishaji hadi kwenye Bandari ya Tanga.

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:
- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kutosha na zenye uwezo kutekeleza kandarasi.
- Hati ya Mlipa kodi ya kampuni ya mwaka uliopita 2022
- Orodha ya kina ya muundo wa mchanganyiko wa zege (Concrete mix Design) na mchanganyiko wa majaribio ya zege (Trial Mix Test) na majaribio ya nyenzo madhubuti za zege (Concrete material Tests).
- Kuzingatia kanuni za mafuta ya petroli za matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Wasambazaji na Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi unapendekezwa sana.

Huu ni wito kwa kuonyesha maslahi au nia (EOI), umekusudiwa kutoa muongozo kwa watoa huduma kuonyesha uwezo na uzoefu kwa kutoa huduma za kuzalisha na kusafirisha vipengee vya zege kwa namna itakayokidhi matarajio ya BBN Limited.

Makampuni yanayovutiwa, yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu barua pepe kwa **procurement@bbnltd.co.tz** (Ukubwa wa barua pepe na viambatanishi: 20 MBs & **Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza) mnamo au kabla ya tarehe 8 Mei 2023, 12:00 jioni, Saa za Tanzania.**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

217389902




RIPOTI YA UCHUNGUZI

## USALAMA HIFADHI ZA TAIFA...

# Kampuni yachimba madini hifadhini

**Na Mwandishi Wetu**

WATENDAJI wa serikali wako njiapanda. Dunia inasubiri kuona hekima yao: Kulinda na kuendeleza Mbuga ya Wanyama Saadani; au kuendelea kuimega kwa kutoa vipande vyake kwa kampuni zilizothibitika kuwa na mwelekeo wa kuharibu mifumo yake ya ikolojia.

Hii ni mbuga ya taifa. Lakini kampuni ya kuchimba chumvi – Sea Salt Limited imemegewa kipande. Kampuni ya kuzalisha sukari – Bagamoyo Sugar Limited imemegewa pia. Mmegaji ni yuleyule – serikali ambayo ni mmiliki wa Mbuga ya Saadani.

Zogo limekuwapo kimyakimya na sasa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere amelikoza upya katika ripoti yake ya mwaka 2020/21 ambamo anabainisha kuwa kampuni iitwayo Sea Salt Limited inachimba madini ndani ya mbuga kwa kutumia leseni Na. ML 05/92.

Sasa hekima inahitajika hapa: Mbuga ya Saadani haipaswi kuwa na mwingiliano wa shughuli zozote za binadamu kama uzalishaji chumvi au sukari. Lakini Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Sea Salt Limited, Ajay Sengar anasema anataka kupanua uzalishaji. Anaomba kuongezwa eneo.

Nani abaki? Nani asogee mbali? Nani aondoke? Ni hekima tu inahitajika kwa kuwa sheria zilishatumika vibaya, ama kwa kutojua au kwa makusudi. Kila mmoja wa washindani anapeperusha karatasi inayoitwa LESENI.

Mwenye eneo kubwa na linalochukua hata jina la eneo lote, ni Hifadhi ya Taifa Saadani (SANAPA) inayosimamia mbuga na yenyewe kusimamiwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Katika ripoti yake, CAG anasema "shughuli za uchimbaji madini husababisha uchafuzi wa mazingira utokanao na kumwagika kwa mafuta yanayotumika kwenye mitambo, takaoevu, uchomaji taka ngumu, na kelele ndani ya hifadhi.

"Kwa maoni yangu, shughuli hizi zinahatarisha mfumo wa ikolojia ndani ya hifadhi na hivyo kusababisha kutokuwapo uhakika wa uendelevu wa Hifadhi ya Saadani."

CAG anapendekeza TANAPA ishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na mamlaka zingine za serikali "kutathmini athari za uchimbaji madini katika mfumo wa ikolojia wa Hifadhi ya Saadani na kuchukua hatua stahiki."

Saadani imezingirwa na halmashauri nne za wilaya za Bagamoyo na Chalinze mkoani Pwani; na Pangani na Handeni mkoani Tanga. Ina ukubwa wa kilomita za mraba 1,100.

Hii ni hifadhi yenye aina 60 za wanyama. Kuna nyani 2,170, nyati 928, turo 730, twiga 654 na tembo 359 (Sensa ya Wanyamapori 2022).

Kuna aina zaidi ya 270 za ndege wakiwamo ndege adimu wanaoitwa Sokoke Pipit, wenye rangi mchanganyiko na ambao hawapatikani sehemu nyingi duniani; na kuna mijusi, kenge na mamba katika mfumo wake wa ikolojia.

Hifadhi imebeba pia samaki, matumbawe – "vichaka-bahari" chini ya maji – ambako samaki hutaga mayai. Kwenye ufukwe wa hifadhi hii ndiko kwenye mchanga unaoitwa "mchanga wa fungani" – ule uachwapo maji yanapokupwa na ambamo kasa wa kijani hufukua na kutaga.

Uzuri na ubora wa Saadani siyo tu wanyama, wadudu na mandhari. Kuna mapato – uchumi. Mwaka 2021/22 peke yake, taifa liliingiza Sh. bilioni moja kutokana na watalii 28,355 waliotembelea mbuga hii.

Yanayoendelea Saadani hivi sasa, yanaibua kumbukumbu za mwaka 1959. Mjerumani aitwaye Bernhard Grzimek, mwanaharakati wa uhifadhi wa asili, aliandika na kutengeneza filamu iitwayo, Serengeti Shall Not Die – Serengeti Haitakufa.

Ujumbe wa filamu ulilenga kuitaka jumuiya ya kimataifa kuchukua hatua za haraka kulinda na kuhifadhi Mbuga ya Serengeti na thamani yake kiikolojia "kwa manufaa ya wakazi wa eneo husika na jamii za kimataifa."

Nani leo ataandika na kutengeneza filamu ya  Saadani Haifi? Na Saadani ni mali, ni fedha, ni ajira, ni kiburudisho kwa watu wa ndani na nje ya nchi. Ni uhai. Hatimaye, ni saadani – jema, zuri, hazina, msaada – tafsiri ambazo jina la mbuga limepewa katika lugha mbalimbali duniani.

Mwekezaji anayechimba chumvi alipewa na serikali leseni ya kuchimba madini kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 2,400.

Kati ya hizo, ekari 728.17 zimeendelezwa bila kibali cha TANAPA, jambo ambalo CAG ameonesha ni kinyume cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, Sura ya 123, Kifungu cha 95(1)(c).

Sheria inatamka kwamba mwenye leseni ya kuchimba madini, chini ya Sheria ya Hifadhi za Taifa ya Mwaka 1959, hatoendeleza ardhi ambayo ni mali ya TANAPA, mpaka apewe idhini na mamlaka hiyo.

Aidha, shughuli nyingine za kibinadamu ambazo zimetajwa kuharibu amani ya mbuga ni pamoja na mifugo – kama vile mbuzi, kuku, mbwa, mingurumo ya mitambo na kelele za binadamu.

Wafugaji mbugani ni miongoni mwa watumishi wapatao 100 katika kiwanda cha chumvi na wakazi wapatao 200 wa Kitongoji cha Makupani kijijini Saadani ambako CAG anasisitiza kuwa "mifugo ina uwezekano wa kuambukiza magonjwa kwa wanyamapori."

Mwandishi anafahamu kuna barua ya tarehe 10 Mei 2021, yenye kumbukumbu Na. AB.2013/222/01/10 kutoka kwa Kamishna wa TANAPA kwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii.

Maudhui ya barua hii yanajenga shaka kuhusu ustawi wa Saadani kutokana na kuwapo shughuli za uchimbaji madini na kilimo ambazo siyo za kihifadhi wala rafiki kwa ikolojia yake.

Lakini ni karibu miaka miwili sasa, hakuna kilichofanyika kurekebisha hali katika mbuga ambayo umaarufu wake unapaa na mapato yake kwa taifa yanaongezeka; huku mazingira yake yakiendelea kutishiwa kiikolojia.

Zogo linalotishia kumega Saadani linafahamika kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa. Novemba 21, 2016 aliagiza kuwekwa alama za mipaka (bikoni) kwenye maeneo ya hifadhi ili kuepusha migogoro ya ardhi.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa SANAPA, Ephraim Mwangomo anasema walitekeleza agizo la waziri mkuu, lakini walipofika eneo lenye mradi wa chumvi, walilazimika kuparuka kuweka bikoni kutokana na utata uliotajwa awali.

Anasema Kamati Teule ya Mawaziri Wanane ilizuru Saadani Oktoba 2019. Hata hivyo, hadi sasa ikiwa ni takriban miaka minne imepita, mgogoro huo haujatatuliwa na wao wanasubiri kutekeleza kitakachoamuliwa na kamati.

Dk. Samuel Gwamaka, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), anakiri kuwa na taarifa za kinachoendelea kati ya SANAPA/TANAPA na mwekezaji wa mradi wa chumvi.

Anasema, "... miezi sita iliyopita nilikwenda kuangalia kinachoendelea; mwekezaji ameomba kuongezwa eneo ili kupanua mradi wake; lakini kuna shida... Tumeagiza kufanyike ukaguzi wa athari za mazingira ili hatua zichukuliwe. Ripoti ya ukaguzi huo ndiyo itakuwa mwongozo wa hatua za kuchukua..."

Makazi ya watu ndani ya mbuga yalianza miaka 48 iliyopita, pale Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) lilipoanza uzalishaji chumvi na kuvuta watu wengi waliosaka ajira na kujenga vibanda kwa ajili ya makazi ya muda.

Kwa mujibu wa John Mbota (56), Mwenyekiti wa Kitongoji cha Makupani, ulipo mradi wa chumvi, makazi yalianza mwaka 1975 pale STAMICO ilipoanza uzalishaji chumvi na kuvutia uhamiaji wa watu waliosaka ajira, hata wakadumisha makazi.


Anasimulia kuwa eneo lenye mgogoro lilitolewa kwa STAMICO na Serikali ya Kijiji cha Saadani. Kufikia mwaka 1986 shirika lilikuwa limejenga kiwanda chake ambacho Mbota anakiri kilikuwa kivutio kwa watu wengi waliosaka ajira; na hatimaye wakalazimika kujenga vibanda ambavyo sasa vingi vimechakaa.


Anafafanua kuwa Kitongoji cha Makupani kawaida kina wakazi 200, lakini msimu wa kuvuna chumvi, idadi huongezeka hadi 800 au zaidi kutokana na shughuli za uvuvi na uvunaji chumvi.

"Changamoto kubwa kwa wakazi ni kuvamiwa na wanyamapori wakali, hasa chui na nyati. Miaka ya karibuni tumekuwa na shida ya chui kuja hapa kwenye makazi ya watu na kuchukua mbuzi. Pia kuna bughudha ya askari wa TANAPA wanapokuwa wanasaka wawindaji haramu," anaeleza Mbota.

Ofisa Ardhi Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze mkoani Pwani, Deo Msilu anakubali kumwonesha mwandishi, nakala ya leseni ya uchimbaji

INAENDELEA UK. 5




Eneo lenye rangi ya njano ndipo ulipo mradi wa chumvi. Kwa mujibu wa leseni iliyotolewa na serikali, eneo hilo lina ukubwa wa kilomita za mraba 9.99.

## HABARI KITAIFA

# Kampuni yachimba madini hifadhini

INATOKA UK. 4

madini Saadani iliyotolewa na Wizara ya Madini mwaka 1992 na kuhuishwa mwaka 2020; ikionesha ramani ya eneo la mradi inavyoingiliana na himaya ya SANAPA.

Msilu anasimulia kuwa eneo lenye mgogoro lilinunuliwa na Sea Salt Limited mwaka 1997 toka STAMICO. Kampuni ya uchimbaji chumvi ilisajiliwa nchini Septemba 4, 1998; na SANAPA ilianzishwa miaka saba baadaye kwa Tangazo la Serikali Na. 281 la tarehe 16 Septemba 2005.

Hata hivyo, kabla ya hapo, eneo hilo lilitengwa kama Pori la Akiba Saadani na kwa maana hiyo, lilikuwa na maslahi maalum serikalini.

Hivi sasa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze inapokea wastani wa Sh. milioni 32 kwa mwaka zikiwa ushuru wa huduma toka kampuni hiyo.

Kaimu Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Saadani, Gabriel Genda anasema kiwanda cha chumvi kimeingia ndani ya maeneo ya mbuga na kwamba ufafanuzi zaidi utatolewa na Kamati Teule ya Mawaziri Wanane inayoshughulikia mgogoro huo.

Mwandishi alipofika ofisi za Wizara ya Maliasili na Utalii jijini Dodoma mwezi uliopita, kupata maelezo juu ya malalamiko hayo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - Wizara ya Maliasili na Utalii, John Mapepele, alimshauri arudi Saadani ili apate maelezo kutoka kwa mtendaji mkuu wa hifadhi.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa SANAPA, Ephraim Mwangomo anasema, wakati hifadhi inaanzishwa mwaka 2005, wakazi wa vijiji vya Saadani na Buyuni waliruhusiwa kuishi karibu na hifadhi "kwa sababu vilikuwapo kabla ya eneo hilo kutangazwa kuwa hifadhi ya taifa.

"Changamoto ni kwamba, ili uvifikie vijiji vya Saadani na Buyuni, lazima upite kwenye mbuga. Hakuna barabara wala njia nyingine ya mkato ya kwenda katika vijiji hivyo. Wakazi wake wanapita bila kulipia.

"Kwa hiyo, Sea Salt Limited imo eneo la STAMICO ambalo limo ndani ya Kijiji cha Saadani, na ili ufike kwenye mradi wao, lazima upitie hifadhini," anafafanua.

Kamishna Mwangomo anasema hifadhi imetoa kibali maalum kwa magari ya mradi wa chumvi, "lakini wageni wao tunawatoza."

Anaeleza kuwa baadhi ya maeneo, hususani uliko mradi huo wa chumvi na maeneo inakopita barabara hiyo, yameathirika, hasa kuhusu ustawi wa viumbe, na sasa yanahitaji kurejeshewa uhalisia.

"Eneo lenye chumvi, kwa maana inakochimbwa au ilikomwagika, majani hayaoti tena. Uliko mradi wa chumvi, kuna mikoko ambayo ni muhimu sana katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Wao walikuwa wanaikata. Mikoko ina uwezo wa kufyonza hewa ukaa mara tano zaidi ya mimea mingine," anaeleza.

Kamishna Mwangomo anasema wamemwambia mwekezaji asikate mikoko, akisema: "Wao hawapendi mvua ili wavune chumvi nyingi; sisi tunataka mvua ili kuwe na majani zaidi hifadhini."

Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Sea Salt Limited, Ajay Sengar anabainisha kiwanda chake kwa sasa kinazalisha asilimia 30 ya uwezo wake, kikiwa kimeajiri Watanzania 93 kati ya wafanyakazi wao 100 (wanawake 30); wakiingizia serikali dola za Marekani 100,000 kwa mwaka kutokana na tani 1,500 za chumvi wanazouza Kenya; kulipa ushuru halmashauri na gharama za TANAPA.

Ripoti ya Takwimu za Msingi Tanzania 2021 iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) Juni 2022, inaonesha uzalishaji chumvi nchini mwaka 2021 ulikuwa tani 112,995. Hii ina maana kwamba, tani 1,500 za chumvi zinazopelekwa Kenya na Kampuni ya Sea Salt Limited ni sawa na asilimia 1.3 ya chumvi yote inayozalishwa nchini kwa mwaka.

Saadani ni hifadhi yenye mifumo mitatu ya kiikolojia; nchi kavu, bahari na mlango wa Mto Wami kwenye Bahari ya Hindi.

**MAPATO YA HIFADHI YA TAIFA SAADANI**

| Mwaka | Watalii | Mapato |
|---|---|---|
| 2019/20 | 13,865 | Mil. 682/- |
| 2020/21 | 20,840 | Mil. 734/- |
| 2021/22 | 28,355 | Bilioni 1/- |

*CHANZO: SANAPA, Machi 9, 2023.*

*KUFAHAMU MADHARA ZAIDI, FUATILIA KESHO.



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule (wa tatu kushoto), akipiga makofi baada ya kufungua maji kwenye bomba la ofisi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tawi la Mivumoni, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ikiwa ni ishara ya upatikanaji wa huduma ya maji baada ya kukamilika kwa mradi mkubwa wa maji wa Bagamoyo hadi Makongo unaotegemea kunufaisha wakazi takribani 450,000 ambao unasimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA). **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE.**

# 1000 waboreshewa maisha Babati

**Na Jenifer Gilla**

WAKAZI takribani 1000 kutoka vijiji 10 vinavyozunguka mapitio ya wanyama ya Kwakuchinja wameboreshewa maisha kupitia mradi wa Mkono kwa Mkono wenye lengo la kuziinua jamii hizo kiuchumi ili kuachana na ujangili wa wanyamapori.

Meneja wa mradi huo unaotekelezwa na kampuni ya utalii ya Chem Chem, Nganashe Lukumay, alisema mpaka sasa wameshatoa fedha kwa vikundi 55 vya Vikoba, Shilingi milioni moja hadi milioni mbili kutegemea na malengo ya kikundi, ambazo wanazitumia kuanzisha biashara ya pamoja kukopeshana ili kupata fedha za mitaji.

Alisema pia wanawapatia mafunzo yatakayowasaidia kuongeza thamani katika shughuli zao wanazozifanya ikiwamo kunenepesha mifugo, elimu ya biashara, ufugaji wa kuku, nyuki, kilimo cha mboga za majani na alizeti.

Nganashe alisema lengo la mradi huo ni kuziwezesha jamii zipate njia mbadala ya kujiongezea kipato tofauti na kutegemea kwenye maliasili kama vile msitu na wanyama hali inayochangia kuongezeka kwa migogoro kati ya binadamu na viumbe hao.

Alisema tangu kuanzishwa mradi huo miaka sita iliyopita wamepata mwitikio mkubwa kutoka kwa wanakijiji ambao wameunda vikundi vya vikoba vyenye asilimia 80 kinamama ambao huongezewa pesa kwa ajili ya kufanya biashara au kukopeshana ili kufanya shughuli binafsi za kiuchumi.

"Tunawapa mtaji kama kikundi kwa ajili ya kuwekeza au kukopeshana ili kila mwanakikundi aanzishe biashara, mwisho wa mwaka wakishavunja kikundi watagawana faida iliyopatikana katika miradi yao na ile fedha tuliowapa inabaki kwenye mfuko kwa ajili ya kuanzia mwaka unaofuata, njia hii imepunguza sana ujangili," alisema.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Upendo, kilichopo Kijiji cha Vilimavili Flora Godson, alisema kupitia mradi huo walipata mkopo wa Shilingi milioni mbili ambazo walizikopesha kwa wanakikundi ili kupata fedha za mitaji ya biashara ndogo.

Alisema mikopo hiyo imesaidia wanawake wa kikundi hicho kuwa na sauti katika familia zao kwa kuwa sasa wanawasaidia waume zako kuendesha familia kwa fedha zinazotokana na biashara wanazofanya jambo ambalo huko nyuma halikuwapo.

"Sasa hivi hata waume zetu wamepunguza ukali na kutuona hatuna thamani kwa kuwa na sisi tunaweka fedha mezani, zamani ilikuwa ukitoa ushauri kwa muwe wako anakuangalia tu kisha anakupuuzia, kwa kweli tunawashukuru Chem Chem kwa kutuinua wanawake," alisema.

Mwanachama wa kikundi hicho, Glosary Mgahawe, alisema mafunzo ya ujasiriamali aliyopata kupitia mradi huo yanamsaidia katika uendeshaji wa biashara yake ya mgahawa na sasa anaweza kurudisha mkopo wa Vikoba kwa wakati tofauti na awali.

"Kabla ya mafunzo nilikuwa sina nidhamu ya fedha, hela nilikuwa nazitumia ovyo bila kuandika kwenye daftari matokeo yake ikifika mwisho wa wiki nakosa hela za marejesho mwisho wa mwaka nafilisiwa na kukosa faida, lakini mafunzo haya yameniweka kwenye mstari nashukuru Mungu," alisema Glosary.

# Mafanikio ya STAMICO yamkosha Msajili Hazina

**Na Mwandishi Wetu**

MSAJILI Mkuu wa Hazina, Nehemiah Mchechu amelipongeza Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) baada ya uongozi wake kufanikiwa kuleta mageuzi makubwa na kulifanya shirika kuanza kuzalisha faida.

Ni mafanikio yanayotajwa wakati mwaka jana shirika hilo lilifikisha miaka 50 tangu kuanzishwa kwake, likitoa gawio la zaidi ya Sh. bilioni 2.2 kwa serikali.

Akitoa wasilisho lake mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati wa Mkutano wa Ofisi ya Msajili wa Hazina na wenyeviti wa bodi, wakurugenzi wa taasisi na mashirika mbalimbali ya umma, Mchechu alisema shirika hilo sasa limeitoa kimasomaso serikali baada ya kuwa moja ya mashirika yanayoingiza faida kubwa kwa serikali.

Alisema lengo la serikali ni kuona mashirika ya umma yanaacha kuwa tegemezi kwa serikali, hivyo kuizidishia mzigo wa kuyaendesha.

Kutokana na mafanikio hayo, shirika hilo ambalo lilitajwa kuwa mfu, mwaka 2019 wabunge walidhibitisha haliwezi kufutwa tena kutokana na mwenendo wa kuridhisha kutokana na utendaji wake na kubadili mtazamo wa awali.

Hayo yanajiri wakati Machi mwaka huu shirika hilo lilitia saini mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya Sh. bilioni 55.2 na Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Dhahabu Geita (GGML) mahususi kwa ajili ya shughuli za kuchoronga miamba ndani ya mgodi huo.

Mkataba huo ulifikiwa baada ya STAMICO kutekeleza kwa ufanisi mkataba wa awali wenye thamani ya Sh. bilioni 5.6 ambao ulitiwa sainiwa Julai 2020.

Kutokana na hali hiyo, Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko alisema mikataba hiyo ni matunda ya uwekezaji uliofanywa na serikali kuhakikisha STAMICO inaimarika na kujiendesha kwa faida.

Pamoja na mambo mengine, shirika hilo linaloongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Dk. Venance Mwasse, limefanikiwa kubuni nishati mbadala ya kupikia 'Rafiki Briquttes' ambayo ni rafiki kwa mazingira.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Simba tunataka rekodi 2003 ijirudie, Yanga inawezekana

**MIAMBA** ya soka nchini Simba na Yanga mwishoni mwa wiki iliyopita, Jumamosi na jana, Jumapili ilishuka dimbani kwenye mechi za kimataifa za mkondo wa kwanza hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba inayobeba dhamana ya kupeperusha bendera ya Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Jumamosi iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Wydad Casablanca ya Morocco katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kwa upande wa Yanga inayoiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, jana ilikuwa ugenini nchini Nigeria ikivaana na wenyeji wao, Rivers United, kabla ya Jumapili ijayo timu hizo kurudiana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Pamoja na kwamba Simba imeanza kwa ushindi, lakini bado kibarua ni kigumu kwao kuweza kuulinda ama kupata matokeo mazuri zaidi katika mchezo wa marudiano utakaopigwa Uwanja wa Mohammed V, nchini Morocco Jumamosi ijayo. Hilo si kwa Simba tu, kwani bila kujali matokeo Yanga iliyoyapata jana nchini Nigeria, nayo inapaswa kujipanga zaidi ili kupata matokeo ya jumla katika mchezo wa marudiano Jumapili na kutinga nusu fainali.

Tunatambua haitakuwa rahisi hasa kwa Simba ambayo itakutana na mabingwa hao watetezi ugenini ambao ni moto wa kuotea mbali wakiwa katika uwanja wao wa nyumbani wa Mohamed wa 5, lakini hilo halipaswi kuogopwa kama wachezaji wataandaliwa vema kiufundi na zaidi kisaikolojia kutokana na namna mashabiki wa wapinzani wao wanavyojua kuisapoti timu yao ikicheza nyumbani.

Katika hilo hatuna shaka kabisa, kwani Simba inajengwa na wachezaji wengi wazoefu waliocheza mechi nyingi za kimataifa wakiwa na klabu mbalimbali lakini pia wakiziwakilisha timu zao za taifa, hivyo suala la mashabiki 'vichaa' wakushangilia mwanzo mwisho wanalijua na hiyo haitakuwa mara ya kwanza kwao kukutana na hali kama hiyo.

Aidha, tunaamini kwa Simba inaweza kabisa kuwatoa mabingwa watetezi hao na haitakuwa mara ya kwanza kwao kufanya hivyo, kwania mwaka 2003, ilifanya hivyo dhidi ya Zamalek baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 hapa nyumbani shukrani zikimwendea Emmanuel Gabriel aliyeizamisha, kabla ya kwenda ugenini, Misri na kupewa kipigo kama hicho lakini ikawatupa nje mabingwa hao wa wakati huo kwa mikwaju ya penalti 3-2 na kutinga hatua ya makundi.

Kama hiyo haitoshi ama ni miaka mingi imepita, mfano wa hivi karibuni tena ikiwa na baadhi ya wachezaji ambao bado wapo katika kikosi cha sasa, mwaka 2019, iliwachapa bao 1-0 Al Ahly wakiwa wa moto, ingawa hawakuwa mabingwa watetezi, mchezo ukiwa ni wa hatua ya makundi, mfungaji akiwa Middie Kagere.

Mwaka 2021, Luis Miquissone akaingoza tena Simba kuichapa Al Ahly katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Wamisri hao wakiwa mabingwa watetezi, hiyo ikiwa ni mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kabla ya mechi ya marudiano nchini Misri, wenyeji nao kupata ushindi kama huo.

Hivyo, suala la Wydad kuwa mabingwa watetezi ama kupata sapoti kubwa kutoka kwa mashabiki wao, hilo halipaswi kupewa nafasi sana zaidi ya kuwaheshimu tu huku kila mchezaji wa Simba akicheza kufa kupona na kuuchukulia kama fainali kwani hata Al Ahly nayo ina mashabiki 'vichaa' wasipoa katika ushangiliaji.

Kwa Yanga, tunaamini itanufaika zaidi kwa kutumia mchezaji wake wa 12 uwanjani, ambaye ni mashabiki, ambapo tunatumia fursa hii kuwataka kujitokeza kwa wingi Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili ili kuwapa sapoti kubwa wachezaji wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






### Muungwana Lazima Nilonge

## Hata timu zikijenga viwanja, makato bado ni yale yale tu

Na Adam Fungamwango

**BAADA** ya kumalizika kwa mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Aprili 16, mwaka huu 'Wekundu wa Msimbazi' wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0, Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), likatoa mahesabu na mchanganuo wake kutokana na watu walioingia, pesa iliyopatikana na mgao wake.

Kifupi ni kwamba watazamaji 53,569 waliingiza kiasi cha Sh. 410, 645,000, na katika pesa hizo zote Klabu ya Simba kama timu mwenyeji inayopaswa kuchukua mapato ya mlangoni kwa mujibu wa kanuni, iliambulia Sh. milioni 188.9

Kitendo cha Simba kuambualia kiasi hicho cha pesa kiliwaibua wadau, mashabiki wa klabu hiyo pamoja na wachambuzi mbalimbali, wakionekana hawaridhishwi na mgao huo.

Umeonekana kuwa ni mgao kiduchu tofauti na mapato yaliyoingia, lakini vile vile makato yalionekana ni mengi mno kwenda maeneo mbalimbali ambayo wanadhani hayastahili na mengine yalikuwa ni makubwa mno.

Umekuwa ni mjadala mkubwa mno kwenye vipindi vya michezo na hata kwenye mitandao ya kijamii, kiasi cha baadhi ya wanachama na mashabiki wa Klabu za Simba na Yanga kusema kuwa suluhisho la mambo haya yote ni kujenga tu viwanja vyao.

Ningependa kuliongelea kidogo hili kwani baadhi ya mashabiki wanaonekana hawaelewi ni kipi kinachoendelea kwenye hili.

Na wanachanganya vitu mbalimbali kwa jambo hili. Sina shaka kabisa na mipango ya Klabu za Simba na Yanga kujenga viwanja vyao kwa kuchezea mechi. Ni jambo ambalo wadau wamelipigia kelele na viongozi wao mra kwa mara wamekuwa wakisema watalitekeleza, lakini hadi leo bado, nadhani muda bado na wanaweza kujenga huko mbele ya safari.

Hata hivyo, niwaambie wanachama na mashabiki kuwa viwanja vijengwe ili klabu ziwe na viwanja vyao, lakini si kuepuka makato. Makato yatakuwa yapo pale pale, na ambayo hayatokuwapo ni gharama za uwanja ambazo zilikuwa ni Sh. milioni 47.2.

Yaliyobaki yote yatakuwapo kama kawaida. Wanachama na mashabiki wengi nimewasikia wakisema kama klabu hizi zingekuwa na viwanja vyao, basi pesa zote hizo zingekuwa za klabu, kitu ambacho ni tofauti.

Cha kuwakumbusha tu hata klabu ikiwa na uwanja wake kama ule wa Azam FC, lakini hazitokwepa makato ya VAT, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), gharama za tiketi, gharama za mchezo, makato kwa TFF, Bodi ya Ligi (TPLB), na FA mkoa.

Kwenye mechi iliyopita, mgao ulikwenda kote huko, hata mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu kati ya timu hizo mbili, makato yalikuwa ni hivyo hivyo, kilichotofautiana hapo kwenye mahesabu yanaanzia mapato ya jumla.

Kinachopatikana kwanza ndicho kinazaa kiasi cha pesa kwenye mgao, kwa sababu mgao na makato yanakwenda kwa asilimia.

Mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara, pesa zipatikane nyingi zaidi kuliko hizo, au chache sana, lakini mgao na makato yanakwenda kwa asilimia na yapo kisheria na kikanuni.

Hapa ndiyo tunarudi kule kule kuwa wadau wengi wa michezo huwa hawataki kujishughulisha kutoa maoni pale TFF wanapokaribisha maoni kabla ya kuanza kwa ligi kila msimu, halafu kitu kikitokea kama hiki baadhi yao ndiyo wanakuwa wa kwanza kupiga kelele.

Kwa wadau wa soka, kama wanataka klabu zibaki na pesa nyingi, wapendekeze kupunguzwa kwa asilimia za makato. Halafu sidhani kama kuna umuhimu wa TFF na Bodi ya Ligi wote kuwa na mgao tofauti. Apewe mmoja tu, halafu wagawane kwa sababu bodi bado iko chini ya TFF. Kuna gharama za tiketi na za mchezo, kwangu mimi zote naona kama ni moja tu. Makato mengine ni ya serikali ambayo hayana mjadala, hata ukijengwa uwanja wako, yapo tu.

Wakati tukitaka klabu zijenge viwanja vyao, tuanzie hapa kwanza, wadau wapendekeze kupunguzwa asilimia kwenye mgao, na gharama zingine kuziunganisha pamoja. Likifanyika hili tunaweza kuona klabu zikipata pesa nyingi hata kwenye viwanja hivi hivi ambavyo si vya kwao. Nina uhakika hata zikijenga viwanja vyao, kwa makato haya, bado wadau watalalamika tu.

# Kampeni msaada kisheria nchini yaiva

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amesema kampeni ya msaada wa kisheria 'Samia legal Aid Campaign' itazinduliwa rasmi Aprili 27, Dodoma na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na kutolewa bure kwa wahitaji nchini.

Alisema lengo la kampeni hiyo ni kutoa elimu kuhusu sheria na haki za msingi pamoja na msaada wa kisheria kwa wahitaji wasiokuwa na uwezo katika nyanja mbalimbali ikiwamo mirathi, migogoro ya ndoa, migogoro ya ardhi na ukatili wa kijinsia.

Vile vile, baada ya uzinduzi huo huduma za msaada wa kisheria zitakuwa zinatolewa kwa wiki 52 tofauti na awali ilikuwa ikitolewa kwa wiki moja kila mwaka.

Dk. Ndumbaro aliyasema hayo jana alipozungumza katika mtandao wa clubhouse ulioandaliwa na Habari Maelezo na kuongeza kuwa kampeni ina lengo la kutambua mchango wa Rais Samia Suluhu Hassan, kupigania masuala ya haki kwa wananchi wake.

Alisema kampeni hiyo imeandaliwa na Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana wadau hasa taasisi mbalimbali zinazopigania haki na kutoa msaada wa kisheria kwa Watanzania hasa wasiokuwa na uwezo wa kulipia huduma huyo.

"Sote tunatambua kuwa hivi karibuni kumekuwa na ukiukwaji wa maadili na uvunjwaji wa sheria ambao umeleta malalamiko mengi sana, kwenye eneo la ukatili wa kijinsia, migogoro ya ardhi, mirathi, haki za binadamu, migogoro ya ndoa na maeneo mengine."

Alisema uchunguzi umegundua Watanzania wengi hawana elimu kuhusu sheria na pia hawafahamu haki zao za msingi jambo linalisababisha wakipata tatizo kutofahamu waelekee wapi kupata msaada wa kisheria na kukosa haki zao.

Kadhalika, juhudi za kutoa msaada wa kisheria zimekuwa zikifanywa na wadau wa kisheria na sekta binafsi kwa muda mrefu, lakini mafanikio yanapatikana kwa kasi ndogo na serikali imeona iongeze nguvu ili kumaliza tatizo hilo kwa pamoja na kwafikia wahitaji wengi.

Alisema ili kufanikisha utoaji wa huduma hiyo wametoa mafunzo kwa wasaidizi wa kisheria 5000, kati ya hao 1,000 wamepewa vyeti ikiwamo mawakili binafsi na taasisi za kisheria.

Alisema kampeni hiyo ni ya miaka mitatu kuanzia ambayo ilianza Februari, mwaka huu, jijini Dar es Salaam na inatarajiwa kumalizika Februari 2026 na kufanya tathmini kujua wapi kunahitaji maboresho ili kuifanya huduma hiyo iwe endelevu.

Alisema baada ya kufanya uzinduzi Dodoma wataacha huduma iendelee na kampeni hiyo itahamia katika mkoa wa Shinyanga, Manyara, Ruvuma, Njombe, Rukwa, Kgoma na Unguja, itarudi Bara, Pemba na kumaliziwa Bara.

Dk. Ndubaro aliwasihi wenye uhitaji msaada wa kisheria na hawana uwezo wa kulipia gharama kujitokeza kwa wingi huduma hiyo itakapofika kwenye mikoa yao kwa kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha kila Mtanzania anapata haki yake kisheria.

# SMZ yashauri kuwatambua wenye mahitaji maalum

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI Zanzibar imetoa wito kwa wadau mbali mbali kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuwatambua wazee, watoto na makundi yenye mahitaji maalum kuwawezesha na kuwatengenezea mazingira rafiki kuonyesha kuwajali.

Wito huo ulitolewa jana na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar Riziki Juma, wakati wa hafla ya kuwakutanisha wazee katika chakula cha pamoja katika kusheherekea Sikukuu ya Eid pili, iliyoandaliwa na Taasisi ya Asma Mwinyi Foundation (AMF), Wilaya ya Mjini Zanzibar.

Waziri Riziki alisema kwa hali na mali Wizara ya Maendeleo ya Jamii jinsia na watoto inashughulikia ustawi wa jamii ya Wazanzibar wote, huku akisisitiza wadau kuungana na serikali katika jitihada za kusaidia wazee, watoto na makundi yenye mahitaji maalum.

"Tuombe na wadau wengine kwasababu kutoa ni moyo na sio utajiri, unapotoa na Mungu anakuongezea zaidi, waone, wajali na wathamini juhudi za wazee wetu hawa, na kuhamasika katika kujitoa kwa ajili ya wazee, watoto na makundi mengine yenye mahitaji maalum," alisema na kuongeza.

"Nitoe shukrani za dhati kwa Mkurugenzi wa AMF, Asma Mwinyi kwa kufikiria kufanya jambo hili kwa kuungana na wazee wetu siku hii ya leo (jana), pia tuendelee kuwajali na kuwatuza wazee wetu, na niombe hili liwe ni kama utamaduni wetu tulifanye kila mwaka, Rais pia anasisitiza wadau kuungana na serikali kwa kuwaleta wazee wetu pamoja," alisema Riziki.

Mkurugenzi wa Taasisi hio, Asma alisema lengo lao kubwa ni kuwasaidia wazee, wanawake, watoto na makundi yenye mahitaji maalum, na kwamba wamewiwa kuwakutanisha wazee katika siku hiyo ili wasijihisi upweke.

"Tumeona watu wengi siku ya Eid pili wanatoka na kwenda maeneo mbalimbali ndio maana na sisi tukaona wazazi wetu na nyinyi kidogo tuje tuwafariji tule kwa pamoja msijisikie upekwe, watoto na wajukuu wenu tupo, pia niwashukuru Serena kwa kutuunga mkono juu ya suala hili ambalo lina maana kubwa kwa wazee wetu," alisema Asma.


**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**TANZANIA ELECTRIC SUPPLY CO. LTD (TANESCO)**

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR CONSULTING SERVICES**

**87.8 MW KAKONO HYDROPOWER PROJECT**

**Tender No. PA/001/2022-2023/HQ/C/05**

**CONSULTANCY SERVICES FOR CONSTRUCTION SUPERVISION AND MANAGEMENT OF THE 87.8 MW KAKONO HYDROPOWER PROJECT IN KAGERA REGION**

**Sector: Energy**

The Government of the United Republic of Tanzania has received financing from the African Development Bank (AfDB), French Development Agency (AFD) and the European Union (EU) towards cost of the 87.8MW Kakono Hydropower Project (HPP), and intends to apply part of the agreed amount to payments under the contract for "consultancy services for construction supervision and management of Kakono HPP in Kagera Region" in the north western part of Tanzania .

The services under this project will entirely include and not limited to the following:

a) Design review of existing feasibility study reports and prepare the associated works bidding documents,
b) Support the client in the procurement of works pertaining to the Kakono HPP,
c) Construction supervision of works comprising:
   i. 87.8 MW Kakono hydropower plant and associated facilities,
   ii. 38.5 km 220 kV evacuation transmission line from the power plant switchyard to the existing Kyaka 132/33 kV substation,
   iii. Uprating the existing substation from 132/33 kV to 220/132/33 kV.

In line with the International Commission on Large Dams, the construction supervision services will be conducted in collaboration with an independent panel of experts. The panel of experts, that is to be recruited separately, will provide support and guidance to the Project Implementation Team on matters pertaining to the construction of the hydropower plant in accordance with international best practices.

The Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO), the client, now invites eligible consultants to indicate their interest in providing these services. Interested Consultants must provide information indicating that they are qualified to perform the services (brochures, description of similar assignments, experience in similar conditions, availability of appropriate skills among staff, etc.).

Consultants may constitute joint ventures to enhance their chances of qualification.
Eligibility criteria, establishment of the short-list and the selection procedure shall be in accordance with the African Development Bank's **"Procurement Policy for Bank Group Funded Operations"** dated October 2015, which is available on the Bank's website at **http://www.afdb.org**.

Interested consultants may obtain further information at the address below during office hours 09.00 – 12.30 hours and 14.00 – 16.30 hours, East African Time, (Monday to Friday) excluding public holidays.

Expressions of Interest must be delivered to the address below during office hours no later than 31 May 2023.

Alternatively, the Expressions of Interest (either unzipped or zipped WINRAR or Winzap shall not exceed 15 MB) may be submitted online via the email sec.tenderboard@tanesco.co.tz, and the password shared via pmu.projects@tanesco.co.tz.

**Attn: The Secretary-Tender Board,**
**TANESCO Umeme Park Building, Ubungo,**
**Ground Floor, Tender Room, Room No. G04,**
**P.O. Box 9024,**
**Dar Es Salaam, Tanzania.**
**Tel: 255 (22) 2451145/2452172; +(255) 782 376147**
**Email: sec.tenderboard@tanesco.co.tz**
**pmuprojects@tanesco.co.tz;**

**Managing Director,**
**Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO)**

217390202



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA' (wa pili kulia), akisalimiana na Katibu Mwenezi mstaafu wa CCM Wilaya ya Muheza, Makame Seif baada ya kumalizika ibada ya Eid El Fitr katika msikiti wa Ijumaa juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mkurugenzi CRDB atajwa viongozi 25 wenye mchango mkubwa kiuchumi

**PORTSMOUTH, Uingereza**

AKIWA na takribani miaka mitano tangu kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela ametajwa na Jarida la African Leadership Magazine (ALM) la Uingereza kuwa miongoni mwa viongozi 25 wenye mchango mkubwa kwenye uchumi.

Tuzo hizo zilizotolewa na kutangazwa mwishoni mwa wiki iliyopita, zilipitia mchakato mrefu ulioihusisha bodi ya uhariri wa gazeti la ALM kutambua majukumu yanayotekelezwa na viongozi wa serikali, kampuni binafsi na mashirika ya kimataifa.

Mhariri Mtendaji Mkuu wa Jarida la ALM, Kingsley Okeke alisema orodha ya viongozi hao imezingatia mchango wao katika uandaaji wa sera rafiki, uongozi makini na programu ziligowagusa na kuwashirikisha wananchi wengi zaidi kwenye uchumi, hivyo kusaidia kuviepuka vihatarishi vilivyojitokeza duniani na kusaidia kuufufua na kuukuza uchumi wa mataifa yao.

"Orodha hii inayowajumuisha mawaziri wa fedha, magavana wa benki kuu na wakurugenzi watendaji wa benki pamoja na taasisi kubwa za fedha barani Afrika imewamulika viongozi waliojitoa kwa upekee kusimamia maendeleo ya mataifa yao hasa kwa kuwawezesha wajasiriamali wadogo kushikiri kujenga uchumi kwa kuwapa fursa za mtaji na nyinginezo licha ya changamoto zinazoshuhudiwa kote duniani&quot," alisema Okeke.

Kuipata orodha hiyo, Okeke alisema kulikuwa na hatua mbili muhimu. Kwanza, ni kutambuliwa kwa viongozi hao kulikofanywa na waandishi nguli wa jarida hilo waliopo katika mataifa tofauti duniani pamoja na wataalamu wa sekta ya fedha Afrika kabla bodi ya ALM kuwachuja na kuwatangaza baada ya kuwapigia kura kwa kuzingatia mambo waliyoyafanya kwenye mataifa yao.

Orodha ya washindi hao imetajwa siku chache baada ya hafla ya viongozi wa uchumi Afrika iliyofanyika jijini Washington DC, Marekani pembezoni mwa mikutano ya mwaka ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani (IMF).

Akizungumzia tuzo hiyo, Nsekela alisema inamtia moyo kuona wadau wakubwa Jarida la ALM wanaona anachokifanya, hivyo ataendelea kuweka mikakati makini kwa kushirikiana na Bodi na Menejimenti ya Benki ya CRDB kuwafikia wananchi wengi zaidi na kuwapa fursa wanazostahili.

Nsekela alisema kuwa tangu kuibuka kwa janga la UVIKO-19, benki imebuni programu kadhaa zilizotekelezwa nchini na kuwagusa wananchi wa kawaida pamoja na kuinua biashara za wajasiriamali kuanzia wadogo mpaka wakubwa.

"Kwa kipindi chote, Benki Kuu ya Tanzania ilikuwa imara ikitoa miongozo iliyoturuhusu tufanye biashara kwa umakini licha ya changamoto zilizokuwapo wakati tukipambana na majanga yote kuanzia UVIKO-19, kupanda kwa bei ya mafuta na sasa vita kati ya Russia na Ukraine," alisema Nsekela.

Ndani ya miaka mitano iliyopita, Benki ya CRDB imetekeleza programu zilizorahisha upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi na sekta ya umma.

Nsekela alisema kuwa ili kuongeza uwezo wa kuwahudumia wajasiriamali wengi zaidi, Benki ya CRDB imekuwa ikishirikiana na wadau kadhaa wa kimataifa kuimarisha mtaji wake. Mwaka jana benki hiyo ilikusanya zaidi ya Sh. bilioni 500 kwa ajili ya uwezeshaji wa wajasiriamali nchini huku mkazo mkubwa ukiwekwa kwa wajasiriamali wanawake.

Benki hiyo pia imekuwa ikichukua hatua ya kupunguza riba kama sehemu ya kusaidia jitihada za serikali kuimarisha uchumi.

Mwaka jana Benki ya CRDB ilipunguza riba kwenye mikopo ya kilimo kutoka asilimia 20 mpaka asilimia tisa, jitihada ambazo zilienda sambamba na kupunguzwa kwa riba ya mikopo ya wafanyakazi hadi asilimia 13.

Nsekela alieeleza kuwa benki hiyo pia imekuwa ikishirikiana kwa karibu na serikali katika kuwawezesha wafanyabiashara wadogo - mamchinga.

Alisema Benki ya CRDB kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetenga Sh. bilioni 60 kwa ajili ya kusaidia kukukuza uchumi wa bluu kwa kutoa mikopo isiyo na riba kwa wajasiriamali wadogo visiwani humo.

Viongozi wengine waliotajwa kwenye orodha hiyo ni Ahmed Shide, Waziri wa Fedha wa Ethiopia; Rindra Rabarinirinarison, Waziri wa Uchumi na Fedha wa Madagascar na Mamadou Moustapha Bâ, Waziri wa Fedha na Bajeti wa Senegal.

Mawaziri wengine ni Zainab Ahmed wa Nigeria, Dk. Renganaden Padayachy wa Mauritius, Samuel Tweah wa Liberia, Matia Kasaija wa Uganda na Adama Coulibaly wa Ivory Coast.

Pia yumo Gavana Lesetja Kganyago wa Benki Kuu ya Afrika Kusini, Johnny Damian wa Benki Kuu ya Sudan Kusini, Dk. Patrick Ngugi Njoroge, Gavana wa Benki Kuu ya Kenya, Dk. Ernest Addison wa Benki Kuu ya Ghana, John Rwangombwa wa Rwanda, Caroline Abel wa Benki Kuu ya Seychelles na José de Lima Massano wa Benki Kuu ya Angola pamoja na Dk. John Mangudya, Gavana wa Benki Kuu ya Zimbabwe.

Rais wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfFB), Dk. Akinwumi Adesina naye ametajwa pamoja na Dk. Adesola Kazeem Adeduntan, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya First ya Nigeria, Mwenyekiti wa Heirs Holding, Tony Elumelu, na Profesa Benedict Oramah, Rais wa Benki ya African Export-Import (Afreximbank).

Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Rokel, Dk. Walton Gilpin nchini Sierra Leone, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Standard Group, Simphiwe Tshabalala, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya BMCE, Othman Benjelloun (Morocco) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Taifa ya Biashara ya Zambia (Zanaco), Mukwandi Chibesakunda.

# 'Mabadiliko Sheria Habari yafanyike kwa upana zaidi'

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Ruvuma (RPC), kimelitaka Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) liongeze kasi kushawishi Bunge lihakikishe mabadiliko ya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 yanafanyika kwa upana zaidi.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Songea juzi, Makamu Mwenyekiti wa RPC, Amon Mtega, alisema kinachofanywa na TEF pamoja na wadau wa habari nchini, kinastahili kuungwa mkono kwa kuwa kinalenga kuiimarisha taaluma ya habari.

Mtega alitoa kauli hiyo kufuatia kauli ya Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, aliyoitoa wiki iliyopita alipozungumza katika mkutano uliowakutanisha wanachama wa TEF na wadau wengine wa habari jijini Dar es Salaam.

"Kwanza kabisa, nianze kwa kuishukuru Serikali ya Rais Samia (Suluhu Hassan) kwa jinsi ilivyoonyesha nia ya kuiboresha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 ambayo imekuwa ikilalamikiwa na wadau wa habari tangu ilipotungwa.

"Pamoja na hayo, ninampongeza Balile, TEF yenyewe na wadau wa habari kwa ujumla kwa jinsi wanavyojitahidi kuhakikisha maoni ya wadau juu ya mabadiliko ya sheria hiyo, yanasikilizwa na serikali pamoja na wabunge kwa ujumla.

"Kwa maana hiyo, ninapenda kuwahahakikishia wadau wa habari wote, kwamba sisi waandishi wa habari wa Mkoa wa Ruvuma, tuko nyuma yao na tunaunga mkono jitihada zao za kuendelea kuishawishi serikali na Bunge ili maoni ya wadau wa habari juu ya mabadiliko ya sheria hiyo, yatekelezwe kwa asilimia kubwa," alisema Mtega.

Kwa mujibu wa Mtega, waandishi wa habari na wadau wa habari, wanatakiwa kushirikiana katika suala hilo kwa kuwa taaluma ya habari ni muhimu kama zilivyo taaluma nyingine muhimu nchini.

Alisema taaluma ya habari ikiendelea kuongozwa na sheria mbovu na kandamizi, nchi haiwezi kuwa na maendeleo sahihi kwa kuwa waandishi wa habari watakuwa wakifanya kazi kwa uoga.

Wiki iliyopita, TEF na wadau wengine wa habari walikutana jijini Dar es Salaam kujadili jinsi serikali ilivyowasilisha bungeni muswada wa mabadiliko ya sheria hiyo wakati wa mkutano wa Bunge wa Januari mwaka huu.

Balile na wadau wengine wa habari, akiwamo Mwenyekiti wa Zamani wa Jukwaa la Katiba Tanzania, Deus Kibamba na Wakili wa Mahakama Kuu ambaye pia ni Mwandishi wa Habari, James Malenga, walisema wataendelea kuishawishi kamati husika ya Bunge pamoja na serikali kwa ujumla, ili maoni ya wadau wa habari juu ya mabadiliko ya sheria hiyo, yatekelezwe kwa upana zaidi.





# Madiwani, watendaji wafundwa kimaadili kuongeza ufanisi

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, wakuu wa idara na vitengo wamepewa mafunzo ya maadili ya viongozi wa umma ili waongeze ufanisi katika utendaji kazi.

Ofisa Maadili ya Viongozi wa Umma Kanda ya Kaskazini, Adam Kuhanda, alisema mjini hapa mwishoni mwa wiki kuwa uzingatiaji wa maadili ni muhimu kwa viongozi wa umma kwa kuwa unawasaidia kufanya vizuri katika utendaji kazi wao.

"Maadili ni kinga kwa viongozi na kuna utafiti umefanyika kuwa asilimia 80 ya mafanikio kwa viongozi yanajengwa na kuzingatia maadili kwa kuwa yanafanya viongozi kuwa waadilifu katika utendaji kazi na kufikia malengo yao," alisema Kuhanda.

Alitaja faida ya maadili kwa viongozi ni pamoja na kuwasaidia kutoa uamuzi sahihi kwa kuwa wawajibikaji kwa uwazi, kufanya kazi kwa pamoja, kupendana, kuheshimiana na kushauriana namna ya kufanya kazi na kufikia malengo waliyojiwekea.

Alivitaja vitendo visivyokuwa vya kimaadili kwa viongozi kuwa ni pamoja na kutumia madaraka vibaya na kujipatia fedha isivyo kihalali, kuweka shinikizo ili mtumishi wa umma afukuzwe kazi kinyume cha sheria na kutumia lugha za matusi.

Alitaja vitendo vingine visivyokuwa vya kimaadili vinajumuisha kuegemea upande mmoja wakati wa kutatua migogoro na kupishana kauli hadharani na kiongozi mwingine.

"Jambo lingine ni kupokea zawadi ya fedha ambazo zinazidi Sh. 200,000 na kuwa chanzo cha kuanzisha migogoro badala ya kuwa kimbilio la suluhisho," alisema Kuhanda.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Jacob Kimeso, alisema mafunzo hayo kwa viongozi yamewagusa vyema na kuongeza tija katika utumishi wao.

Kimeso aliwataka viongozi, madiwani na watumishi wote wa halmashauri hiyo wayazingatie mafunzo hayo ili yawaongoze katika utumishi wao kwa wananchi.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Simanjiro, Kiria Laizer, alisema mafunzo hayo yatawafanya viongozi hao kubadilika na kutimiza wajibu wao ipasavyo.

"Mafunzo kama haya yanapaswa kufanyika mara kwa mara ili viongozi wakumbushwe wajibu wao katika kuwatumikia wananchi kupitia serikali inayoongozwa na CCM," alisema.



Mkuu wa Polisi kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Leonard Bandora (kushoto), akitoa elimu ya usalama barabarani kwa madereva wa bajaji katika barabara ya kwenda Hospitali Teule ya Muheza, juzi. Kulia Mkuu wa Operesheni za polisi wa wilaya hiyo, Edwin Musiba. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mabilioni yanusuru wanafunzi kukosa madarasa na madawati

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KAIMU Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Hargney Chitukuro, amesema kuwa mwaka huu, hakuna mwanafunzi aliyekosa kuingia darasani kwa kukosa chumba cha darasa au dawati.

Amesema wamefanikiwa kuepukana na adha hiyo kutokana na uamuzi wa serikali kutoa zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na samani zake.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wakati wa uzinduzi wa vyumba vinne vya madarasa vilivyojengwa kwa Sh. milioni 80 katika Shule za Sekondari Kaloleni, Chitukuro, kiongozi huyo alisema fedha za ujenzi wa madarasa hayo ni sehemu ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 100. "Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha hizi ambazo kwa jiji letu tumejenga madarasa 100. Kati yake, 20 ni ya ghorofa ambayo yako Sekondari ya Elerai vyumba vinne, Terati vyumba vinane na Ungalimitedi vyumba vinane," alisema.

Vilevile, alibainisha kuwa walipatiwa na serikali fungu lingine Sh. milioni 940.9 kutoka mradi wa Boost. Wanazitumia kujenga vyumba vya madarasa na vyoo kwenye Shule za Msingi Msasani, Muriet, Sinoni, Terati, Uhuru na Ukombozi.

Alisema pia wamepokea fedha kutoka Hazina Sh. milioni 980 kujenga shule mbili mpya za Nafco na Korongoni za msingi pamoja na ujenzi wa vyumba tisa vya madarasa katika Shule ya Msingi ya Mchepuo wa Kiingereza ya Arusha (3), Naura (2), Meru (2) na Ungalimitedi (2). Alisema ujenzi wa miradi hiyo unatarajiwa kukamilika Juni 30 mwaka huu, akiutaja utasaidia wanafunzi kukaa bila msongamano na kuongeza ufaulu.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alisema kukamilika kwa ujenzi wa madarasa hayo na kuendelea kwa ujenzi mwingine wa shule mpya na vyumba vya madarasa ni ishara ya ushirikiano wa viongozi mkoani hapa. Alisema Rais anapambana kujenga na kuboresha miundombinu ya shule ili wanafunzi wapate elimu, hivyo ni vyema kila mmoja akamuunga mkono kuhakikisha kila mtoto anapata elimu bila kisingizio chochote.

# Taasisi yalaani ukatili kwa watoto, mapenzi jinsia moja

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MKURUGENZI wa Kituo cha Kulea Watoto cha Goodwill and Humanity Foundation, Sayyed Idarusi, amesema taasisi hiyo inalaani na kupinga vikali ndoa ya jinsia moja na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na kinamama.

Idarusi alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini hapa alipobainisha namna walivyopingana na vitendo hivyo na kuitaka jamii kutokubali kushiriki kwenye mambo hayo kwa kuwa siyo utamaduni wa kitanzania.

Vilevile, alisema wanataka kuieleza dunia kwamba taasisi hiyo haikubaliani na matendo hayo na wako mstari wa mbele kulaani ndoa za jinsia moja na vitendo vya ukatili ambavyo vimekuwa vikifanywa dhidi ya watoto na kinamama.

"Taasisi hii tunalaani ndoa za jinsia moja na hatuungi mkono mambo hayo kwa kuwa moja ya huduma tunazotoa ni kuhifadhi watoto waliopotea na waliofanyiwa ukatili na tuna ofisa ustawi maalum anayeambatana na maofisa wa serikali kuwapeleka mahakamani wanaowafanyia ukatili watoto.


"Tumekuwa tukipokea watoto wengine wamekatwa masikio, mikono, waliounguzwa kwa moto, waliovuliwa nguo na kumwagiwa maji ya moto na kuwababua ngozi. Hayo ni matatizo makubwa wanayokumbana nayo watoto," alisema.

Aliongeza kuwa wanaungana na kauli ya serikali ya kukataa ukatili dhidi ya watoto kwa kuwa ukatili huo na ndoa za jinsia moja havikubaliki na havipaswi kufumbiwa machi.

Msimamizi wa Casa Della Giaio, Consolata Mgumba, aliitaka jamii kupunguza ubinafsi na kurudisha moyo wa kujali na kuwaangalia watu wengine.

"Tujiulize watoto yatima kwanini zamani hawakuwapo? Familia tumeacha kutekeleza majukumu yetu na tumekimbilia kuwapeleka watoto kwenye vituo hivyo," alionya.

Alitaka jamii kuzingatia maadili kwa kuwa mambo ya ushoga yanatokana na baadhi ya familia kutengana na watoto wakajikuta wanalelewa na mzazi mmoja peke yake.





# Wazazi wasita kuandika wosia wangali hai

**Na Marco Maduhu**, GEITA

BAADHI ya wananchi Mtaa na Kijiji cha Mpomvu, Kata ya Mtakuja, Halmashauri ya Geita Mji, wameonesha kutokukubaliana na suala la uandishi wa wosia wa mali zao wakiwa hai huku wakiomba elimu zaidi kutolewa kutokana na suala hilo kuonekana kuwa kinyume na taratibu walizozoea.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kuhusu suala hilo, wananchi hao walisema licha ya elimu ambayo inaelezwa kusaidia kuondoa migogoro ya ardhi wanayokutana nayo hususani ndugu wakati wa kugawana mirathi, bado kuna umuhimu wa kuelimishwa zaidi kwa kuwa suala hilo ni geni kwao.

Charles Mtasima, Mkazi wa Mpomvu alisema; "elimu ambayo tumeipata ya msaada wa kisheria tutaitumia ipasavyo katika kutatua migogoro yetu mbalimbali ikiwamo ya ardhi, lakini kuhusu kutoa wosia bado kuna haja ya kuongezewa uelewa kwani hatujazoea kufanya hivyo na sio utamaduni wetu."

Awali, Mwanasheria kutoka Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa vitendo (LEAT), Clay Mwaifani, ambaye pia ni Ofisa Miradi, akizungumza wakati wa kutoa elimu ya msaada wa kisheria kwa wananchi wa maeneo hayo alisema, mzazi kuandika wosia sio kwamba anajitakia kufa, bali ni utaratibu mzuri wa kuepusha vurugu na mafarakano katika familia pale atakapo fariki.

"Nawaombeni wazazi mjenge tabia ya kuandika wosia bado mkiwa hai, hakuna kesi ngumu kama za kugombania mirathi sababu mwenye mali tayari ameshafariki, na migogoro hii ya mirathi inafikia hatua mbaya sana hata ya kushikiana mapanga, sasa tunataka tutoke huko siku ukifariki familia ibaki na amani," alisema Mwaifani.

Aidha, alisema wakati wa kuandika wosia hatakiwi kuoneshwa mtu yeyote iwe ni siri ya mzazi na mwanasheria wake au wakili ili siku akifariki wakati wa vikao vya familia anafika na kuonyesha wosia ambao uliachwa na mwenye mali hizo kwa lengo la kuacha familia na maelewano.

Aliitaka jamii pia wanapokuwa na migogoro ya aina yoyote wasipende kujichukulia sheria mkononi, waende kwenye vyombo vya sheria ili kusuluhishwa kwa amani na kila mtu apate haki yake.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Mpomvu, Mathias Samwel, alipongeza utolewaji wa elimu hiyo ya msaada wa kisheria na kuwataka wananchi wanapokuwa na migogoro wasijichukulie sheria mkononi, watumie sheria kutatua matatizo yao huku akiwataja watu wa vikundi vya kukopeshana kuwa na migogoro ya mara kwa mara.



Wafanyakazi wa kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), wakisafisha ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ikiwa ni sehemu ya lengo kuu la bia ya Rockshore kwenye jamii la kuweka fukwe zote safi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima watahadharishwa ununuzi holela mbolea

**Na Timothy Itembe**, MARA

WAKULIMA mkoani Mara wametakiwa kufuata utaratibu wa ununuzi wa mbolea ya ruzuku na kutahadharishwa kuepuka kununua kwa bei zisizo sahihi kunako sababisha vitendo vya utapeli kutokana na kuuzwa kwa Sh.70,000.

Tahadhari hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Lameck Borega, wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Mara kuwa serikali imeweka ruzuku hiyo ili kumnusuru kila mkulima nchini na gharama ya mbolea.

Alisema mbolea hiyo inatakiwa kuuzwa kwa bei elekezi ya Sh. 70,000 kwa mfuko wa kilo 50 huku akiwataka wakulima kutoa taarifa kwa wote watakaouza kwa bei zaidi na kuahidi kuwachukulia hatua za kisheria.

"Lengo ni kuwakwamua wakulima na kuongeza kasi ya uzalishaji wa sekta hiyo inayotegemewa na wananchi wengi na moja kati ya malengo ya Wizara ya Kilimo ni kufikia mwaka 2030 kuendelea kutoa ruzuku ya mbolea mpaka pale itakaposhuka bei kwenye soko la dunia ili kuwapunguzia gharama za uzalishaji na wakulima nchini," alisema Borega.

Meneja Mkuu wa Chama cha Ushirika cha wakulima wa Mkoa wa Mara, WAMACU, Samweli Gisiboye, alisema mkakati wao ni kuhakikisha wakulima wanapata mbolea kwa misimu yote miwili ili kupandisha kiwango cha uzalishaji katika kilimo.

Alisema kufikia Aprili 15, 2023, wamegawa mbolea kwa wakulima mifuko 19,800 sawa na tani 990 kwa kushirikiana na kampuni za mbolea OCPT na TFC.

Makamu Mwenyekiti WAMACU, Michael Mugwewa, alisema mpaka sasa wana kahawa kilo 208,125 na kuwataka wakulima kuendelea kuwa na imani na chama chake katika suala zima la kuuza zao hilo kwa bei ya sokoni iliyopitishwa na mkutano mkuu wa chama hicho.

## Vijana kupata ajira ujenzi jengo la NHC

**Na Shaban Njia**, KAHAMA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), limeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la kisasa la kibiashara katika eneo lao la uwekezaji, Kata ya Bukondamoyo, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga utakaogharimu Shilingi bilioni moja huku likitarajia kutoa nafasi za ajira kwa vijana wanaozunguka eneo hilo hususani zisizohitaji ujuzi.

Hayo yamebainishwa juzi na Meneja wa Shirika hilo Mkoa wa Shinyanga, Angelina Magazi, wakati wa ukaguzi wa eneo la ujenzi wa jengo hilo kuwa mradi umeanza kutekelezwa na kuahidi kuajiri vijana wanaozunguka eneo hilo kwa ajira zisizo na utaalamu.

Alisema jengo hilo litakuwa na vyumba vikubwa vya maduka 84, migahawa, 'SuperMarket' na sehemu ya kuoshea magari na watawapangisha wateja watakaokidhi masharti kwa gharama nafuu lengo likiwa ni kusaidia ajira kwa vijana.

Alisema, utekelezaji wa mradi huo umeanza na unatarajia kukamilika katika kipindi cha miezi sita ijayo na hiyo itakuwa ni fursa kwa watu kupangishwa kwa gharama nafuu.

Meneja mradi kutoka NHC, Mhandisi Mburuga Matamwe alisema, ujenzi wa mradi huo ni uwekezaji mkubwa ambao haujawahi kufanyika mkoani Shinyanga na watahakikisha unakamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma kwa wananchi wa eneo hilo hususani wafanyabiashara watakaohitaji vyumba vya biashara.

Msanifu wa mradi huo, Robart Kintu alisema, mradi upo jirani kituo kidogo cha mabasi Bukondamoyo na eneo la uwekezaji la viwanda vidogo na vikubwa maarufu kama Dodoma na vijana watapewa kipaumbele katika ajira zisizokuwa na utalamu na wachuuzi watafanya biashara zao kipindi chote cha ujenzi.

Ferister Joram, mkazi wa eneo hilo alisema, watafurahi kama watapewa kipaumbele katika ajira za muda ikiwamo kuchota maji, kusogeza vifaa vya ujenzi kwa mafundi kwani baadhi ya miradi inatekelezwa na kuajiri vijana kutoka nje ya mkoa.

Nipashe
# Spotika



MAKOCHA 5 WALIOWAZIBA MIDOMO WAKOSOAJI WAO UK. 12-13



ALPHONSO DAVIES

# WALINZI WA5 BORA WA KUSHOTO MSIMU HUU

**LONDON,** England

KATIKA enzi ya kisasa ya mpira wa miguu, nafasi ya beki wa kushoto imebadilika sana. Sio tena mabeki watetezi, mabeki wa pembeni sasa ni sehemu muhimu ya timu yoyote inayopenda mashambulizi. Mabeki bora zaidi wa kushoto leo wana uwezo wa kutengeneza nafasi za kufunga, kuinua uwanja kwa kasi, mbinu na ufahamu wa kimbinu.

Ni lazima wawe na uwezo wa kulinda vema huku pia wakicheza jukumu muhimu katika mchezo wa kujenga mashambulizi.

Iwe wanavuka mpira au kupiga pasi zenye kusisimua katikati ya safu ya ulinzi, beki wa kushoto wa kisasa ni mchezaji mwenye ujuzi wa hali ya juu ambaye anaweza kuwa tofauti kati ya mafanikio na kushindwa katika mchezo.

hapa tunawangalia mabeki watano bora wa kushoto kwenye soka msimu huu, twende sasa...

**#5 Theo Hernandez (AC Milan)**

Theo Hernandez anasogea uwanjani kama mtu anayejua haswa anakoenda. Mwendo wake unasisimua, ukungu wa rangi nyekundu na nyeusi anaposhuka chini ya ubavu wa kushoto, akiwaacha mabeki katika kuamka kwake.

Mpira unaonekana kushikamana na miguu yake kama gundi, kugusa kwake kwa uhakika na kujiamini. Haishangazi kwamba amekuwa mtu muhimu kwa AC Milan, mchezaji mwenye uwezo wa kubadilisha mkondo wa mechi kwa mafowadi.

Hernandez amethibitisha kuwa mahiri katika pande zote mbili za uwanja na amekuwa mmoja wa mabeki bora zaidi wa kushoto duniani kwa miaka kadhaa sasa. Katika mechi 35 za mashindano yote akiwa na AC Milan hadi sasa msimu huu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, amefunga mabao matatu na kutoa asisti tano.

**#4 Luke Shaw (Manchester United)**

Mnamo 2015, Luke Shaw alivunjika mguu katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya PSV Eindhoven, ambapo ilihatarisha kipaji chake. Alitumia karibu mwaka mmoja nje ya dimba, akifanyiwa upasuaji mara nyingi na ukarabati mkubwa kabla ya kurudi kwenye soka la kulipwa.

Inashangaza kwamba Shaw tangu wakati huo ameingia na kuwa mchezaji ambaye yuko leo baada ya jeraha hilo baya. Uwezo wa Muingereza huyo wa kuendeleza mpira ni wa hali ya juu na ustadi wake wa kupiga krosi unaendelea kuimarika.

Ushambuliaji wa mbele wa Shaw ni kipengele muhimu cha mchezo wa Manchester United. Pia ni beki wa kutegemewa anayeweza kufuatilia kwa haraka na kujilinda dhidi ya wapinzani wagumu zaidi.

Katika mechi 37 kwenye michuano yote aliyoichezea Manchester United hadi sasa msimu huu, Shaw amefunga bao moja na kutoa asisti sita.

**#3 Oleksandr Zinchenko (Arsenal)**

Katikati ya nyota wote wa Manchester City, Oleksandr Zinchenko hakuwahi kuonekana kama mchezaji ambaye anaweza kuwa na athari kubwa kwa timu yoyote kwenye Ligi Kuu. Hata hivyo, amethibitisha kuwa ni mchezaji muhimu akiwa Arsenal katika kipindi cha msimu huu baada ya kujiunga nao msimu uliopita wa majira ya joto.

Matokeo ya Zinchenko ya bao moja na pasi mbili za mabao katika mechi 29, yanaweza kukufanya uamini kuwa hana matokeo mengi. Lakini haiwezi kuwa mbali zaidi na ukweli. Ingawa nyota huyo wa kimataifa wa Ukraine alianzia benchi mara nyingi huingia ndani na kujiunga na safu ya kiungo ya katikati ya uwanja.

Ustadi wake mzuri na usahihi wa kucheza mpira umekuwa muhimu kwa uchezaji wa Arsenal msimu huu. Zinchenko amewashika mashabiki kwa uwezo wake wa ajabu wa kiufundi na akili ya mchezo na amekuwa mmoja wa wachezaji wenye ushawishi mkubwa kwa Arsenal msimu huu.

**#2 Alphonso Davies (Bayern Munich)**

Akiwa beki wa kushoto wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Canada, Alphonso Davies ana kasi ya kipekee na mwepesi, ambayo humwezesha kufunika sehemu nyingi za ardhini kwa kujilinda na kujiunga na mashambulizi.

Ana udhibiti bora wa mpira na anacheza vizuri kwenye nafasi zake na kumfanya kuwa mali muhimu katika kumiliki mpira.

Ufahamu wake wa ulinzi na ufahamu wa nafasi humruhusu kupunguza ipasavyo vitisho vya kushambulia vya wapinzani, huku ustadi wake wa kukera na upigaji krosi kutoka upande wa kushoto unaweza kutengeneza nafasi nyingi za kufunga kwa timu yake.

Mchanganyiko wa Davies wa ustadi wa kushambulia na ulinzi unamfanya kuwa mmoja wa mabeki bora wa kushoto katika soka la dunia leo. Beki huyo wa kushoto mwenye umri wa miaka 22, amefunga mabao matatu na kutoa pasi nane za mabao katika mechi 35 katika michuano yote hadi sasa msimu huu.

## ISIKUPITE

HAT-TRICK aliyofunga Riyad Mahrez juzi, Jumamosi dhidi ya Sheffield United wakati Manchester City ikishinda 3-0, inakuwa ya kwanza kwenye hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA tangu mwaka 1958.



**#1 Raphael Guerreiro (Borussia Dortmund)**

Raphael Guerreiro amekuwa msaada mkubwa kwa Borussia Dortmund msimu huu. Ubora wake wa kuvutia zaidi ni ustadi wake wa kushambulia, kwani ni mpiga chenga bora na mpiga pasi mbunifu wa mpira.

Mbio za Guerreiro na uwezo wa kuungana na wachezaji wenzake katika nafasi ya tatu ya mwisho humfanya kuwa tishio mara kwa mara katika mashambulizi. Ingawa anajulikana sana kwa mchango wake wa kushambulia, Guerreiro pia ni beki dhabiti mwenye uwezo mzuri wa kukaba.

Pia, amecheza sana katika safu ya kiungo ya kati msimu huu na amefanya kazi nzuri katika nafasi hiyo mpya. Beki huyo wa kushoto wa Ureno, amefunga mabao matano na kutoa asisti 13 katika mechi 30 za michuano yote hadi sasa msimu huu akiwa na Borussia Dortmund.

# MAKOCHA 5 WALIOWAZIBA MIDOMO WAKOSOAJI WAO

**LONDON,** England

MSIMU wa 2022-23 umekuwa wa ufufuo na ukombozi. Klabu za juu za Ulaya ambazo hazijafanya vema katika misimu ya hivi karibuni ama zimerejea katika ubora wao au zimejifufua msimu huu.

**Hata hivyo, mafanikio yao yametokana na makocha wao wa hali ya juu, ambao si tu kwamba wamebadili falsafa katika klabu hiyo, lakini pia wamejenga tabia na molari ya ushindi.**

Makocha ndio uti wa mgongo wa klabu yoyote, na mafanikio ya msimu huanza na kumalizika nao. Hata hivyo, kumekuwa na baadhi ya makocha katika misimu ya hivi karibuni ambao wamekuwa wakibezwa sana.

Lakini kuna wachache ambao wamethibitisha uwezo wao kwa usimamizi na ujuzi wa kimbinu msimu huu.

Kwa maelezo haya, sasa tuwaangalie makocha watano ambao wamewanyamazisha wale wote waliokuwa wanawabeza msimu huu...

### #5 Unai Emery - Aston Villa

Msimu wa Aston Villa 2022/23, umekuwa chini ya rada, huku klabu hiyo kutoka Jiji la Birmingham ikiwa katika mbio za kufuzu kuwania kucheza Ligi ya Europa msimu ujao.

Baada ya kuambulia pointi tisa pekee katika michezo 11 ya kwanza ya Ligi Kuu, timu hiyo ilifikisha alama 41 katika michezo 22. Sasa wapo katika kinyang'anyiro cha kufuzu kwa mashindano ya Ulaya msimu ujao. Lakini kuibuka upya kumekuwa chini ya Unai Emery, ambaye aliondoka Villarreal na kujiunga na Villa Novemba mwaka jana.

Emery anafahamu wazi jinsi timu zake zinapaswa kucheza. Ingawa inahitaji mbinu makini, bosi huyo wa Hispania ameweza kuweka hali ya nidhamu katika timu ambayo ilikuwa kwenye hali ngumu chini ya Gerrard.

Ollie Watkins amecheza mbele kwa kujitolea na kufunga mabao 14 ya ligi msimu huu. Jacob Ramsey amekua na kipaji kizuri, wakati wachezaji kama Ezri Konsa, Douglas Luiz, Emiliano Martinez, na John McGinn wametoa msingi mzuri kwa upande mwingine. Kwa hiyo kila mchezaji anacheza kwa uwezo wake, shukrani kwa mfumo mzuri uliotumiwa na Emery.

Mhispania huyo atafurahishwa na timu yake, haswa baada ya mbinu zake kukosolewa na mashabiki kadhaa wa Arsenal wakati alipokuwa kule Emirates. Lakini tangu wakati huo, Emery amejidhihirisha akiwa Villarreal na sasa amerejea Ligi Kuu England na kuwaziba mdomo wale wote waliombeza.

### #4 Eddie Howe - Newcastle United

Utajiri wa Newcastle United ulilazimika kubadilika mara tu baada ya kuchukuliwa na Mfuko wa Uwekezaji wa Umma (hazina ya utajiri wa nchi ya Saudi Arabia).

Lakini ni wachache waliotarajia klabu hiyo kuwania nafasi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa haraka sana. Shukrani kwa Eddie Howe, nyakati nzuri zimerejea, wameamka na wananguruma tena.

Ingawa sera yao ya kuajiri imekuwa nzuri, kocha huyo Muingereza mwenye umri wa miaka 45, amekuwa sababu kuu ya maendeleo makubwa ya klabu hadi sasa.

Wakati alipokuwa Bournemouth, mbinu za kushambulia za Howe zilisifiwa mara kwa mara. Hata hivyo, amepata uwiano sawa Newcastle, na timu kuwa na ulinzi thabiti na nguvu ya kusisimua ya kushambulia.

Kuongezwa kwa Bruno Guimaraes, Dan Burn, Alexander Isak, Nick Pope, na wengine kadhaa katika kipindi cha miezi 18 iliyopita, kumechangia kwa kiasi kikubwa kwenye hili. Kuibuka tena kwa wachezaji kama Miguel Almiron na Joe Willock pia kumekuwa ufunguo wa maendeleo ya klabu msimu huu.

Huku timu hiyo ikishika nafasi ya nne kwenye jedwali zikiwa zimesalia mechi nane pekee msimu kukamilika, Howe amethibitisha ubora wake katika soka la England msimu huu.

### #3 Xavi Hernandez - Barcelona

Xavi Hernandez ameleta mapinduzi makubwa katika Klabu ya Barcelona msimu huu, hasa baada ya kushindwa kushinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, katika misimu minne iliyopita. Lakini mambo yamebadilika sasa. 'Blaugrana' hao wametawala takriban kila mechi za ligi msimu huu na inastahili pointi 11 mbele ya Real Madrid iliyo nafasi ya 2 kwa sasa.

Hili limewezekana tu kutokana na mabadiliko ya mbinu ya Xavi, huku kocha huyo akitanguliza ubabe katika safu ya kiungo. Mara nyingi amechagua kuwapanga viungo wanne kati ya Frenkie de Jong, Sergio Busquets, Franck Kessie, Gavi, Pedri, na Sergi Roberto.

Hii imewawezesha kutawala mpira katika michezo mingi, huku wachezaji kama Ousmane Dembele, Raphinha, na Robert Lewandowski wakiwa wamejiweka sawa mbele ya lango.

Safu ya ulinzi pia imepangwa, huku Ronald Araujo akicheza nafasi ya nyota nyuma msimu huu. Ameongoza safu ya ulinzi kwa ustadi, na kuibuka kwa Alejandro Balde katika beki wa kushoto pia imekuwa nyongeza nzuri.

Wakosoaji wengi walitilia shaka sifa za usimamizi za Xavi wakati wa uteuzi wake kwani hapo awali alikuwa ameiongoza Al Sadd nchini Qatar. Hata hivyo, hatimaye amekuwa mzuri kwa klabu yake ya utotoni na atatafuta kuipeleka Barcelona kileleni mwa mashindano ya Ulaya msimu ujao.

### #2 Jose Mourinho - AS Roma

Jose Mourinho bila shaka ndiye kocha mkuu zaidi wa karne ya 21, mataji na sifa zake zinajulikana wazi.

Tangu alipowasili kwenye eneo la tukio baada ya kuiwezesha FC Porto kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2004, bosi huyo wa Ureno hajageuka nyuma. Alifanya vema akiwa Chelsea kwa kutwaa mataji mawili huku pia akishinda mataji matatu akiwa na Inter Milan. Muda wake akiwa Real Madrid pia ulikuwa wa kustaajabisha, ingawa hakuweza kushinda Kombe la Ulaya akiwa nao.

Hata hivyo, alipokea shutuma nyingi kwa mbinu zake za kizamani za ulinzi wa "kupaki basi" wakati alipokuwa Manchester United na Tottenham Hotspur. Kwa hiyo, wachache walitarajia mzee huyo wa miaka 60, asingerejea kwenye ubora, lakini Mourinho amefanya hivyo. Tangu achukue mikoba ya AS Roma msimu wa majira ya joto wa 2021, ameleta mabadiliko katika klabu hiyo.

Nyongeza za Tammy Abraham, Roger Ibanez, Paulo Dybala, Nemanja Matic, na wengine kadhaa zimeleta uthabiti na ustadi wa kushinda michezo. Mbinu yao ya kushambulia imekuwa ya moja kwa moja zaidi, na safu yao ya ulinzi ni ngumu sana, na kuwafanya kuwa timu ngumu kucheza dhidi yao.

Sifa hizi ziliwafanya kushinda Kombe la Ligi ya Europa Conference mwaka jana, na kwa sasa wako nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A. Timu hiyo ya Italia haijashiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu msimu wa 2018-19, jambo ambalo Mourinho amekuwa akitaka kulibadilisha tangu achukue nafasi hiyo.

Mbinu za bosi huyo wa Ureno zinaweza kuwa za kisayansi kidogo kwenye Ligi Kuu, lakini kwa hakika amevunja kanuni tena katika soka la Italia. Mtu maarufu kwa kupata mambo makubwa akiwa na watu wa chini, Mourinho hakika bado ni mmoja wa makocha bora katika soka la dunia.

### #1 Mikel Arteta - Arsenal

Ikiwa kuna timu moja katika soka ya dunia ambayo imefanya zaidi ya matarajio yote msimu huu, hakika ni vijana wa Mikel Arteta, Arsenal.


Wakati Edu na Arteta wamekuwa wakijenga mradi huu kwa uthabiti na kwa busara katika miaka miwili iliyopita, kazi yao imeleta mafanikio katika msimu wa sasa. Tangu siku ya kwanza ya msimu wa 2022-23, Arsenal imekuwa na hali ya ndani ya kujiamini, nia na molari ya kuzishinda timu pinzani.

Wachezaji kama Bukayo Saka, Martin Odegaard, Oleksandr Zinchenko, Granit Xhaka, na Aaron Ramsdale wametoa msingi kwa timu kwa kutoa maonesho ya 9/10 wiki baada ya wiki.

Kuongezwa kwa Gabriel Jesus na Zinchenko majira ya joto, pamoja na kuwasili kwa Jorginho na Leandro Trossard, pia kumeiwezesha Arsenal kuendeleza changamoto ya ubingwa.

Lakini hakuna hata moja ya mambo haya ambayo yangewezekana bila mbinu za Arteta. Mhispania huyo amehimiza timu yake kuwa na jeuri zaidi, hesabu, molari na busara katika maeneo yote ya uwanja. Iwe kupitia pasi za haraka, za kusisimua kati ya mistari au kuwafundisha mawinga wake jinsi ya kupokea mpira, mfumo wa Arteta umekuwa usio na dosari.

Kitu ambacho pia amefanikiwa kukimiliki ni kutengeneza safu ya ulinzi inayojiamini na bila mpira na haina hofu ya kucheza safu ya juu. Kwa mtu ambaye alikosolewa vikali hadi mwisho wa msimu uliopita, Arteta hakika amewanyamazisha wapinzani wake msimu huu, jambo ambalo bila shaka anaweza kujivunia.



BUKAYO SAKA
MIKEL ARTETA

## Nukuu

"Nina uzoefu pale Palmeiras (ya Brazil) ilipokaa bila kutwaa ubingwa kwa miaka 20, hapa ni sawa kabisa. Ndio maana nimekuja, sisemi tutashinda ubingwa wa ligi kwa sababu hakuna kilichoamuliwa bado, lakini tupo pale. kupigana hadi mwisho," **Mshambuliaji wa Arsenal, Gabriel Jesus, akiionya klabu yake ya zamani, Manchester City kuhusu mbio za ubingwa Ligi Kuu England.**




"Mimi ni shabiki mkubwa wa Aaron Ramsdale [kipa wa Arsenal]. Ikiwa utakuwa mzungumzaji na mkali kama Ramsdale, lazima uunge mkono na kiwango chako, kwa sababu vinginevyo yote yanaonekana kuwa ya kuchekesha. Kweli, anafanya hivyo na ananikumbusha Peter Schmeichel. Ni wazi kwamba Ramsdale anapaswa kuendelea kuboresha ili kufikia viwango vya Schmeichel, lakini kifurushi kizima kinamfanya kuwa kitu cha karibu ambacho nimekiona kwa muda mrefu," **mshambuliaji wa zamani wa Manchester United na Everton, Wayne Rooney.**




"Kwa klabu yoyote, kwa timu yoyote, kwangu hilo halikubaliki. Kama kocha siwezi kukubali kwamba timu yangu haitoi ubora wake. Timu, watu binafsi ... sitakubali kamwe. Ndiyo, bila shaka, ninawafanya wafahamu uchambuzi wangu ulikuwa nini, hisia zangu kuhusu mchezo huo zilikuwa nini, madhara yangu ya mchezo yalikuwaje. Hawakuendana na viwango vya jinsi ninavyosimamia timu katika soka ya kulipwa." **Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag, baada ya timu yake kutupwa nje na Sevilla kwa jumla ya mabao 5-2 kwenye hatua ya robo fainali ya UEFA Europa.**





MSIMU wa 2022–23 umekuwa wa ufufuo na ukombozi. Klabu za juu za Ulaya ambazo hazijafanya vema katika misimu ya hivi karibuni ama zimerejea katika ubora wao au zimejifufua msimu huu.

Uk. 12&13



Straika wa Simba, Jean Baleke, akiukwamisha mpira wavuni mbele ya mabeki wa Wydad Casablanca na kipa wao Youssef El Motie juzi kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa. **MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA INAVYOTISHA KUTOA VIPIGO MABINGWA WA CAF

**Na Adam Fungamwango**

JUMAMOSI iliyopita ilikuwa ni mwendelezo wa Klabu ya Simba kuwabwaga Mabingwa wa Afrika, ikiwa kwenye ardhi yake ya nyumbani wa Benjamin Mkapa, ikiweka rekodi nyingine ya kushinda mechi zake dhidi ya Mabingwa Watetezi na safari hii ikiwa zamu ya Wydad Athletic Club kutoka Casablanca nchini Morocco kuangukia pua kwa bao 1-0.

**Katika mchezo huo wa mkondo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, straika raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Jean Balele aliingia kwenye orodha ya wachezaji waliofunga mabao dhidi ya mabingwa wanaokufa wakija nchini Tanzania, alitupia bao pekee dakika ya 30 ya mchezo.**

Kama nilivyoeleza kuwa hii imekuwa ni kama utamaduni sasa kwa Simba kushinda dhidi ya timu ambazo zinatetea kombe hilo, kwani imeshawahi kufanya mara kadhaa bila kuangalia matokeo ya mechi zake za ugenini, ambapo mara moja imeshawahi kufuzu.

Si kwa Mabingwa wa Afrika tu, hata Mabingwa wa Kombe la Washindi kwani mwaka 1985 katika hali iliyowashangaza wengi iliwachapa Al Ahly ya Misri ambao walikuwa ndiyo watetezi wa kombe hilo.

Ikiwa inalitetea kombe lake la Washindi Afrika lililolichukua mwaka 1884, mechi za 16-bora, Al Ahly ilishuka nchini na ikacheza na Simba kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, ikaangukia pua kwa kuchapwa mabao 2-1.

Mechi hiyo ilichezwa Agosti 22, 1985, Al Ahly ikianza kupata bao dakika ya tano lililofungwa na Mohamed El Khatib 'Bibo', ambaye ndiye alikuwa anatoka kuchukua tuzo la mchezaji bora wa Afrika wakati huo na kwa sasa ndiye Mwenyekiti wa Klabu hiyo, lakini 'Golden Boy', Zamoyoni Mogella, straika hatari kipindi hicho, alisawazisha dakika ya 44 na katikati ya kipindi cha pili, kiungo Mtemi Ramadhani alifunga bao la pili.

Hata hivyo, Simba ilitolewa kwenye michuano hiyo kwa jumla ya mabao 3-2 ilipokwenda kufungwa 2-0 nchini Misri.

Katika makala haya, tunaziangalia mechi ambazo Simba ilipata ushindi nyumbani ikicheza na Mabingwa wa Afrika...

**Simba 1-0 Zamalek**

Ilikuwa ni Mei 18, 2003 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam (sasa Uhuru), Simba ilipocheza na bingwa mtetezi wa Afrika.

Simba ilishinda bao 1-0 lililowekwa wavuni na straika Emmanuel Gabriel, ambapo pamoja na ushindi huo hakuna aliyeweza kuamini kuwa ingeweza kusonga mbele hasa ikijulikana kuwa inakwenda kucheza kwenye nchi ya Misri iliyokuwa ikisifika si kwa soka tu kwa timu zake, lakini hata mashabiki wenye vituko na vurugu, pamoja na mambo mengi ya nje ya uwanja.

Kwa sababu mechi hiyo ndiyo pekee ambayo Simba iliweza kuwatoa mabingwa watetezi, tuiangalie upande wa pili ilipokwenda kucheza ugenini Juni Mosi mwaka huo huo jijini Cairo dhidi ya mabingwa hao watetezi.

Yeyote aliyetegemea Simba ingefungwa mabao mengi haikuwa hivyo. Ilifungwa bao 1-0 lililowekwa wavuni na nahodha wao wakati huo, Hazem Emam.

Timu hizo zikalazimika kwenda kupigiana mikwaju ya penalti ambapo Simba iliivua ubingwa Zamalek kwa kushinda penalti 3-2. Kipa Juma Kaseja aliibuka kuwa shujaa, akiokoa penalti za Wael El Qabbani, Beshir el Tabei na Mahmoud Abdelrazek Hassan, maarufu kama Shikabala.

Simba iliivua Zamalek ubingwa na kutinga hatua ya makundi, kwani wakati huo ilikuwa ni hatua ya raundi ya pili, baada ya kwanza kuitoa Santos ya Afrika Kusini kwa mikwaju ya penalti pia, kutokana na suluhu mechi zote mbili.

**Simba 1-0 Al Ahly**

Simba ilipangwa Kundi A na Mabingwa Watetezi Afrika, Al Ahly, ilipofanikiwa kuingia hatua ya makundi mwaka 2021.

Mabingwa hao wa Afrika walikuwa wanatoka kucheza Ligi ya Mabingwa wa Dunia dhidi ya Bayern Munich ya Ujerumani.

Wakiwa wa moto, Al Ahly ilikumbana na kipigo cha bao 1-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, lililowekwa wavuni na winga raia wa Msumbiji, Luis Miquissone. Mechi hiyo ilichezwa Februari 23 mwaka 2021. Ushindi huo ulikuwa ni moja kati ya rekodi ya Simba kuwafunga mabingwa wa Afrika. Inawezekana ilikuwa rahisi kwao kwa sababu msimu uliopita 2019/20 walikuwa wote kwenye kundi moja. Na pia msimu huo Simba ilishinda bao 1-0 Februari 12 kwa bao lililofungwa na Meddie Kagere, ingawa wakati wanacheza mechi hiyo Al Ahly haikuwa bingwa. Timu hizo zilikuwa Kundi D.

**Simba 1-0 Wydad Casablanca**

Kwa mara nyingine tena, Simba juzi ilifanya ilichokifanya huko nyuma, baada ya kuichapa Wydad bao 1-0 kupitia kwa Mkongomani Baleke.

Imerudia kama ilivyofanya miaka miwili nyuma. Kinachosubiriwa sasa ni mechi ya marudiano itakayopigwa Aprili 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Mfalme wa Tano nchini Morocco. Wanachama na mashabiki wa Simba hawahitaji kile kilichofanywa miaka miwili iliyopita kwa sababu tayari kimeshafanyika. Wanachohitaji ni kile kilichofanyika miaka 20 iliyopita jijini Cairo kwa kuwavua ubingwa Zamalek.

## JE, WAJUA?



NI Liverpool na Manchester United pekee - ambazo zimeweza kutwaa FA Cup na ubingwa wa Ulaya kwa msimu mmoja - zikifanya hivyo mara mbili. Kwa msimu huu tayari Manchester City imetinga fainali ya FA Cup na nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Je, nayo inaweza kuingia katika rekodi hiyo?



## Ujenzi mnara Mashujaa awamu ya kwanza kugharimu bil. 1/-

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UJENZI wa Mnara wa Mashujaa kwa awamu ya kwanza jijini Dodoma, unatarajia kugharimu kiasi cha Shilingi bilioni moja huku Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, akiwataka wataalam kuujenga kwa viwango na ubora.

Akizungumza katika kikao na wataalam, wakurugenzi na wakuu wa vitengo mbalimbali, Waziri Mhagama alisema mnara huo unatarajiwa kukamilika mapema kabla ya maadhimisho ya siku ya Mashujaa mwaka huu ili kutoa fursa kwa wananchi ya kujifunza mambo mbalimbali yaliyofanywa na Mashujaa hao kipindi hicho.

Mhagama aliwataka wataalam kushirikiana vyema na makandarasi ili ujenzi ukamilike katika viwango vya ubora vilivyokusudiwa na serikali. "Hakikisheni Mnara huu unajengwa katika viwango vya ubora, lakini pia ukamilike kwa wakati ikiwamo kutumika kwenye siku ya mashujaa wananchi waweze kuona," alisema Mhagama.

Waziri Mhagama alisema ujenzi wa mnara huo kwa awamu ya kwanza ni moja ya jitihada zinazofanywa na serikali na kwamba wataalam wanapaswa kutekeleza ujenzi huo ipasavyo na kuongeza kuwa matarajio yao ukamilike mapema kabla ya maadhimisho ya Mashujaa mwaka 2023.

"Kukamilika kwa mnara huu itakuwa ni hatua kubwa sana kwa serikali kama sehemu ya kuwakumbuka mashujaa wetu jinsi walivyoipigania nchi yetu na utakuwa wa kipekee sana na nembo kubwa kwa Makao Makuu ya nchi yetu Dodoma," alisema Mhagama. Alifafanua kuwa kupitia mnara huo Watanzania watapata fursa ya kutembelea na kujifunza mambo mengi mazuri yaliyofanywa na Mashujaa wakati wakipigania taifa lao.

Hata hivyo, Waziri Mhagama alisisitiza matumizi sahihi ya fedha zilizotolewa na serikali kukamilisha ujenzi huo, kuhakikisha zinatumika kama ilivyopangwa.

Alisema pia kukamilika kwake kutafungua fursa nyingi za kiuchumi kutokana na miundombinu rafiki na huduma muhimu zitakazowekwa katika mnara huo.

Aidha, amebainisha kwamba ujenzi wa mnara huo ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa wakati wa maadhimisho ya siku ya mashujaa yaliyofanyika Julai 2022 na kuagiza kujengwa kwa mnara wenye ubora na hadhi ya makao makuu ya nchi.

# Watanzania watakiwa kuungana kupiga vita mmomonyoko maadili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kusimama pamoja kama taifa kupinga vitendo vya ushoga, ndoa za jinsia moja, ulawiti na usagaji badala ya kuwaachia jukumu hilo viongozi wa dini na serikali pekee yao.

Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, alisema hayo juzi jijini hapa wakati akitoa hotuba yake kwenye ibada ya swala ya Eid el Fitr, iliyofanyika katika Msikiti wa Gadafi.

"Ni jukumu la kila Mtanzania kukemea mambo mabaya na kuhamasisha matendo mema, inatupasa kusimama pamoja kama taifa kuhakikisha kuwa mambo haya ya hovyo ambayo mataifa ya nje wanataka kutuletea tunayapinga kwa kuwa ni kinyume na mila na desturi zetu," alisema Shekhe Rajabu.

Alisema pamoja na kuwa mambo hayo ni kunyume na mila za kitanzania pia ni kinyume na maagizo ya Mungu kwa mwanamume kumuoa mwanamume mwenzake au mwanamke kuolewa na mwanamke mwenzie.

"Mambo haya ambayo yanataka kuletwa katika nchi ni mambo ya kumchukiza Mungu, ambayo hata mnyama hawezi kufanya kwani ni kunyume na uumbaji wake, haiwezekani leo mwanamume aolewe na mwanamume mwenzake au mwanamke amuone mwanamke mwenzake," alisema Rajabu.

Aliwataka Watanzania kuacha tabia ya kupokea kila kitu kinachoingizwa nchini na mataifa mengine kwa kuwa hali hiyo inaweza kusababisha kuongezeka kwa vitendo vya mmomonyoko wa maadili.

"Mmomonyoko wa maadili hivi sasa umekithiri nchini kutokana na kuiga mambo ambayo sio mila na desturi zetu hali ambayo inasababisha kuongezeka kwa vitendo vya maasi nchini ikiwamo baba kulawiti watoto wao wa kuwazaa, wanandoa kuuana pamoja na mauaji katika jamii zetu," alisema.

Pia, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais Dk. Philp Mpango na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa kusimama imara kueleza hisia zao waziwazi za kupinga vitendo hivyo vya ushoga na ndoa za jinsia moja nchini.

"Nawapongeza sana viongozi wetu wa ngazi ya juu wakiongozwa na Rais wetu kipenzi, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kupinga hadharani vitendo hivi vya ndoa za jinsia moja kuingia nchini na sisi hatuna budi ya kuwaunga mkono kupinga kwa pamoja vitendo hivi vya laana," alisisitiza.

Naye, Imamu wa msikiti wa Area 'C', Hilali Abdullaziz, akitoa hotuba ya swala ya Eid el Fitri iliyofanyika katika uwanja wa Jamuhuri jijini hapa, alisema vitendo vya ushoga vinapaswa kupigwa via na kila mtu.

"Vijana wengi sasa hivi hawaoi unawezakuta sababu ni hii ya ushoga, lazima tuhakikishe kuwa haya mashirika ambayo inaelezwa kuwa yanasaidia kueneza ushoga tunayapinga mara moja kama taifa ili kuokoa vizazi vyetu kwenye hatari hii ya ushoga," alisema Abullazizi.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akizungumza na waumini baada ya Ibada ya Jumapili katika Nyumba ya Malezi ya Mtakatifu Yosefu, Miyuji Jimbo Kuu Katoliki Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Singida yanunua magari mawili kuzoa taka

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Singida, imenunua magari mawili ya kuzoa taka yaliyogharimu zaidi ya Sh. milioni 200 ikiwa ni mkakati wa manispaa hiyo kuhakikisha mji unakuwa katika hali ya usafi.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Jeshi Lupembe, alisema jana kuwa magari hayo ambayo yatazinduliwa na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, yamenunuliwa kwa fedha za mapato ya ndani zilizotengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Alisema kupitia mapato hayo ya ndani Manispaa inajenga Kituo cha Afya Mtipa kwa Sh.milioni 500, kujenga machinjio ya kisasa Sh. milioni 120, kujenga jengo la utawala ghorofa tatu eneo la Karakana fedha kutoka Serikali Kuu, Shilingi bilioni moja na Sh. milioni 31 zimetumika kulipa fidia ya dampo Mwankoko.

Lupembe amewaomba wananchi wa Manispaa ya Singida kutoa ushirikiano kwa kuhifadhi taka kandokando ya barabara ili magari hayo yatakapopita yaweze kuzichukua. "Jukumu ya kuuweka mji katika hali ya usafi ni la wananchi wote na sio la watendaji wa Manispaa, haipendezi kuona mtu anatupa taka ovyo barabarani, sasa tumenunua haya magari tuyatumie ili kuuweka mji wetu kwenye usafi," alisema Lupembe.

Aidha, Lupembe alihimiza wananchi kufanya usafi maeneo ya kaya zao na kupanda miti minne kila kaya, kulipa ada ya taka Sh. 2000 na wafanyabiashara Sh. 5000 kwa mwezi ili kudumisha usafi wa mji na kuboresha mazingira.

Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Manispaa ya Singida ilitangaza kutumia zaidi ya Sh. milioni 701.6 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ununuzi wa magari ya kuzolea taka, fedha ambazo zimetokana na mapato ya ndani.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa Singida, Serukamba aliwataka wananchi wa Manispaa ya Singida kuhifadhi taka za majumbani mwao badala ya kuzitupa barabarani au kuzipeleka kwenye majalala huku Halmashauri ya Manispaa hiyo ikiagizwa kuweka utaratibu wa kupita kila kaya kukusanya taka hizo.



HABARI MBEYA

# Wakulima wapendekeza kubadili mfumo tozo maendeleo

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAKULIMA wa kahawa wa Kanda ya Mbeya (Songwe, Rukwa na Mbeya) wameiomba serikali kubadili mfumo wa kukusanya tozo ya maendeleo ya zao hilo kutoka Sh. 200 kwenye kila kilo moja ya kahawa na ikusanywe kwa viwango vya asilimia.

Wakizungumza kwenye kikao cha wadau wa kahawa wa kanda hiyo kilichofanyika mwishoni mwa wiki jijini hapa, baadhi ya wakulima hao walisema kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya bei ya kahawa kuna wakati tozo ya Sh. 200 kwa kila kilo ya kahawa inamuumiza mkulima.

Benjamin Mwambungu, mkulima wa zao hilo kutoka Mbozi, mkoani Songwe alisema ipo haja kwa serikali chini ya Bodi ya Kahawa kupitia upya tozo hiyo na kuamua kupanga viwango kwa mtindo wa asilimia ili kutomuumiza mkulima.

"Wakati tozo ya Sh. 200 inapangwa, bei ya kahawa aina ya arabika ilikuwa Sh. 6,000 kwa kilo moja, kama ingeendelea kuwa bei hiyo mpaka mwisho wa msimu isingekuwa shida sana, lakini bei hushuka hadi kufikia Sh. 4,000 kwa kilo moja huku tozo ikibakia kuwa ile ile ya Sh. 200 jambo ambalo sasa linageuka kuwa maumivu kwa wakulima," alisema Mwambungu na kuongeza, "Sisi wakulima tunapendekeza tozo hii ikusanywe kwa mtindo wa asilimia ili kama bei ikiongezeka na tozo nayo inaongezeka na ikishuka tozo pia inapungua jambo litakalotoa unafuu kwa mkulima na kuhakikishia serikali mapato yake," alisema Mwambungu.

Daudi Simkoko, mkulima wa kahawa kutoka Busokelo, wilayani Rungwe, alisema bei ya kahawa wakati mwingine inatofautiana katika mkoa mmoja na mwingine, lakini wote wanatozwa kiwango sawa cha tozo ya maendeleo ya kahawa.

Alisema kuna wakati bei ya kahawa inakuwa juu mkoani Songwe kutokana na msimu wa mauzo kuwahi, na unapoanza mkoani Mbeya bei inashuka, lakini wakulima wote wanatozwa kiwango sawa cha tozo ya maendeleo ya zao.

"Inapotokea hali ya bei kutokuwa sawa, sisi tunaona kuna wakulima wanaumizwa kuliko wengine ili kuleta usawa ni vizuri tozo hii ikapangwa kwa asilimia badala ya kuwapo kwa kiwango cha aina moja cha Sh. 200.

Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Kahawa Tanzania, Kajiru Kisenge, alisema ameyachukua maoni hayo na atayafikisha katika ngazi husika kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Hata hivyo, Kisenge alisema tozo hiyo ina manufaa makubwa katika uendelezaji wa zao la kahawa kwa kuwa inakusudia kutumika kutatua changamoto nyingi zinazowakabili wakulima.

Kwa msimu uliopita pekee fedha hizo zimetumika kuzalisha miche ya kahawa na kusambaza kwa wakulima na kupunguza au kumaliza kabisa kero ya muda mrefu ukosefu wa miche.

Alisema endapo tozo hiyo utaendelea kukusanywa ipasavyo, inakusudiwa kutumika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hususan ukame uliokithiri na kuathiri mazao ya wakulima.

Alisema serikali itarajia kutumia fedha za tozo ya maendeleo ya kahawa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji kwa kujenga mabwawa yatayotumiwa na wakulima kumwagilia mikahawa yao wakati wa ukame.

Akiongoza kikao hicho cha wadau wa kahawa kwa niaba ya Mkuu wa mkoa, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Benno Malisa, aliitaka Bodi ya Kahawa kushughulika kero nyingi walizonazo wakulima wa Kahawa ili zao hilo liwe tija.

Alisema zao hilo linawanufaisha wakulima kiuchumi, lakini pia lina mchango mkubwa katika pato la taifa kwa kuingiza fedha za kigeni nchini.

Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Songwe, ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, Ester Mahawe aliwataka wakulima wa Kahawa kutumia uwezo wao wote kuongeza uzalishaji ili kujikwamua kiuchumi.

Kanda ya Mbeya inazalisha zaidi ya asilimia 54 ya kahawa yote inayozalishwa nchini.



Katibu wa Elimu, Malezi na Mazingira wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM Wilaya ya Kinondoni, Johnson Kashasha (mwenye kanzu katikati) na Mwenyekiti wa Wazazi Kata ya Wazo, Jesca Mrope (wa pili kushoto) na viongozi wengine, wakiwa na watoto yatima wanaolelewa katika Kituo cha Babu na Bibi cha Nguzo Madale, baada ya futari iliyoandaliwa na jumuiya hiyo kata mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOHN BADI**

# Apendekeza usalama barabarani kuingizwa kwenye mitaala

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

KAMANDA wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, SP Yusuph Kamotta, ameiomba Wizara ya Elimu kuingiza kwenye mtaala somo la usalama barabarani ili wanafunzi kuanzia shule ya awali hadi Sekondari wajifunze matumizi sahihi ya barabara na sheria zake.

Alisema hatua hiyo itawasaidia watoto kujifunza sheria mbalimbali za usalama barabarani na kuepukana na ajali.

Alitoa ombi hilo juzi alipozungumza na wadau wa usalama barabarani mkoani hapa kuwa moja ya mikakati ya kukabiliana na ajali ni kuandaa kizazi cha watoto ambao watapata elimu itayowasaidia kuwa mabalozi wazuri hapo baadaye.

"Pamoja na mikakati mizuri ya serikali kukabiliana na ajali kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya barabara, reli na anga, tunahitaji pia kuandaa kizazi cha baadaye ambacho kitakuwa ni balozi mzuri ya kuepusha ajali, ni wakati sasa somo la usalama barabara kuingizwa kwenye mtaala wa elimu na watoto wetu wafundishwe kuanzia ngapi ya awali mpaka sekondari," alisema SP Kamotta. Akizungumzia suala hilo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa alisema, atafanya kikao cha maofisa elimu kuangalia jinsi litakavyotekelezwa.

Alisema suala hilo ni muhimu kwa kuwa litasaidia kuwaepusha watoto na ajili za barabarani kwa sababu watakuwa wamejifunza sheria mbalimbali zitakazowaongoza wakati wanatumia barabara.

"Hili ni jambo muhimu kwa ajili ya usalama wa watoto wetu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa waathirika wa ajali, wanapovuka barabara au wakiwa kwenye vyombo vya moto, ntafanya kikao na maofisa elimu tuone suala hili linatekelezeka vipi," alisema Malisa.

Alisema licha ya baadhi ya shule kuwa mabalozi wa usalama barabarani, uhitaji wa elimu ni muhimu kutokana na baadhi ya madereva kutoheshimu sheria za barabara hata kama wanafunzi wakiwasimamisha ili wavuke barabara.

# Mchungaji mbaroni tuhuma kutoa taarifa za uongo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MCHUNGAJI wa Kanisa la Pentecost Neno lililo hai, Mbarikiwa Mwakipesile, mkazi wa Isyesye jijini Mbeya, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mkoa wa Mbeya kwa tuhuma za kutoa taarifa za uongo kupitia mtandao wa kijamii akimtaja Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa kuwa ndiye aliyemuua mwanawe.

Mchungaji Mwakipesile anadaiwa Machi 8, alitoa taarifa kupitia mtandao wa YouTube kwamba Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa ndiye aliyeratibu kifo cha mwanawe aitwaye Wokovu.

Upande wa Jamhuri ulisema kuwa mchungaji huyo alisikika kwenye mtandao huo akisema "Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa aliyepo sasa ndiye aliyeratibu mipango ya kumuua mtoto wangu" alinukuliwa.

Waendesha Mashtaka upande wa Jamhuri wakiongozwa na Dominic Paul, wamesema mshtakiwa alieleza hayo huku akijua wazi kwamba ni maelezo ya uongo na ni kinyume na kifungu namba 16 cha sheria ya mitandao namba 14 ya mwaka 2015.

Mshtakiwa Mwakipesile baada ya kuulizwa na mahakama kuhusu tuhuma hizo alikanusha na kutimiza masharti ya dhamana ya mdhamini mwenye mali isiyohamishika yenye thamani isiyopungua Sh. milioni 10.

Hakimu Mkazi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya, Peter Scout, aliahirisha kesi hiyo hadi Mei 4, 2023 kwa ajili ya kusomwa hoja za awali na baadaye kesi hiyo kuanza kusikilizwa.

Baada ya kumaliza taratibu za kimahakama Mchungaji alipokewa na waumini wake mahakamani hapo waliofika kufuatilia mwenendo wa kesi hiyo ya jinai namba 10 ya mwaka 2023.



# Utengenezaji boti za uvuvi washika kasi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWEKEZAJI wa Kampuni ya Quiro Group, Yang Hao inayotengeneza boti kwa ajili ya uvuvi, imeahidi kuongeza kasi ya ujenzi wa boti hizo kwa ajili ya Serikali ya Zanzibar ili kufikia malengo ya kukuza uchumi wa bluu.

Raia huyo wa China anayefanyia kazi zake Zanzibar, alitoa ahadi hiyo jana wakati wa hafla ya kuwatunuku zawadi wafanyakazi bora wa kampuni hiyo sambamba na kusherehekea Sikukuu ya Eid el Fitr huko ofisini kwake Amani, Zanzibar.

Alisema kampuni yake ni miongoni mwa kampuni zilizopata tenda ya serikali kutengeneza boti za uvuvi na ukulima wa mwani ili kuwawezesha wavuvi na wakulima wa mwani kufanya shughuli zao kwa ufanisi na kujipatia kipato.

Alisema ubora wa kazi na viwango ni muhimu ambao umeiwezesha kampuni kupata tenda nyingi zaidi za utengenezaji wa boti Zanzibar na Tanzania Bara.

Alisema uwezo na ubunifu umewezesha kampuni hiyo kuwatunuku wafanyakazi wake bora wanne ambapo kila mmoja alipewa zaidi ya Sh. milino tatu.

"Nimefurahishwa na utendaji kazi wa wafanyakazi wangu ambapo boti tunazotengeneza zimeonekana kuwa na ubora na viwango vinavyokubalika na taasisi mbalimbali," alisema Yang, maarufu Makame Mchina.

Mwekezaji huyo pia alipongeza Wizara ya Uchumi wa Bluu kwa kumpatia tenda ya kutengeneza boti 500 za uvuvi na ukulima wa mwani ambapo mafanikio hayo yamemwezesha kupata tenda nyingine ya kutengeneza boti kubwa za uvuvi zenye urefu mita 14.

"Hivi sasa nimepokea tenda nyingine kutoka Wizara ya Uvuvi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutengeneza boti kubwa za uvuvi, kazi ambayo kwa sasa ninaendelea nayo," alisema.

Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi na Mkuu wa Upepelezi Kituo cha Polisi Mwanakwerekwe, Wilaya ya Magharib B Unguja, Abdul-hamid Muhammed, aliwataka wafanyakazi wa kampuni hiyo kuwa na uadilifu na uaminifu na kuwa tayari kuwafichukua watu wanaofanya hujuma kiwandani.

"Mmepata nafasi ya kufanya kazi kiwandani hapa, hivyo muwe waaminifu katika kulinda mali za kampuni na inapotokea vitendo vya hujuma, msiogope kutoa taarifa," alihimiza.

Ali Yussuf Ali na Said Muhammed Said, wafanyakazi bora wa kampuni hiyo, walisema wamefurahishwa na uamuzi wa kampuni wa kuwatunuku zawadi kwa kufanya kazi vizuri. Walisema fedha walizopatiwa watazitumia kujikwamua kiuchumi kwa kuazisha biashara ndogo ambazo zitawaongezea kipato.

"Ninampongeza mwekezaji wa kampuni hii kwa kutuamini na kutupatia zawadi hii ambayo ameitoa wakati mwafaka," alisema Said.



Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni inayotengeneza boti za uvuvi ya Quiro Group, Yang Hao (wa pili kulia), akikabidhi nyama kwa mfanyakazi wake, Muhammed Said katika hafla ya ugawaji nyama kwa wafanyakazi wa kampuni hiyo, kwa ajili ya Sikukuu ya Eid El Fitr, eneo la Amani viwanda vidogo Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

## Wizi mifugo waishtua serikali

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, amezitaka kamati za ulinzi za mkoa kujipanga vizuri kwa ajili ya kukabiliana na wezi wa mifugo kwa kuwa wanarudisha nyuma juhudi za wafugaji. Mahmoud aliagiza hayo mwishoni mwa wiki alipokutana na kamati za ulinzi za mkoa kujadili suala la wizi wa mifugo baada ya kupata malalamiko mengi ofisini kutoka kwa wananchi.

Alizitaka kamati hizo kufanya kazi zake vizuri kwa kushirikiana na masheha wa shehia mbalimbali ambao pamoja na wananchi ni rahisi kuwatambua wahalifu.

Pia aliwataka wakazi wa mkoa huo kurudisha ulinzi shirikishi katika kukabiliana na matukio ya uhalifu kwa sababu kamati zenyewe na vyombo vya ulinzi ikiwamo Jeshi la Polisi, peke yao hawawezi kukabiliana na matukio hayo.

"Wito wangu kupitia kamati za ulinzi za mkoa na wilaya, wahakikishe wanafanya kazi ya kuwasaka wahalifu wanaojishughulisha na wizi wa mifugo na kurudisha nyuma juhudi za wafugaji," alisema.

Baadhi ya Masheha wamekiri kuwapo matukio ya wizi wa mifugo ambayo wahalifu hutekeleza uovu wao nyakati za usiku.

Sheha wa Kilombero, Wilaya ya Kaskazini Unguja, Mwanahamisi Ali Silima alisema tayari wana matukio sita yaliyoripotiwa katika shehia yake na hakuna mhalifu aliyekamatwa.

Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini Aunguja, Unguja Sadifa Juma Khamis alisema wamejipanga kwa kushirikiana na kamati za ulinzi na Jeshi la Polisi kupambana na wizi wa mifugo.

# Ulaya yaongoza kutoa watalii wanaotembelea vivutio Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BARA la Ulaya limeongoza kwa kuwa na watalii wengi walioitembelea Zanzibar kwa mwezi wa Machi mwaka huu, likitoa wageni 35,564 waliofika visiwani hapa.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari mwishoni mwa wiki kuhusu uingiaji wa wageni kwa mwezi wa Machi, Mkurugenzi Rasilimaliwatu, Mipango na Utawala kutoka Kamisheni ya Utalii, Aviwa Issa Makame, alisema idadi ya watalii wote waliongia nchini kwa mwezi uliopita ni 45,915.

Akitoa taarifa hiyo katika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, alisema idadi hiyo inaonyesha uingiaji wa wageni umepungua kulinganishwa na mwezi Febuari ambao walikuwa 65,430.

Alisema wageni waliofikia Zanzibar wanatoka sehemu tofauti lakini Bara la Ulaya linaongoza likifuatiwa na Bara la Afrika ambalo lilitoa wageni 4,892, likifuatiwa na Bara la Amerika wageni 2,941 na Bara la Asia wageni 256.

Aviwa alisema nchi tano zilizoongoza kwa wageni walioingia nchini ni Italia wageni 5,929, Ufaransa 4,559, Ujerumani 4,083, Czech 3,030 na Poland 2,753.

Alisema wageni 41,271 waliofika visiwani hapa, walitumia usafiri wa anga kupitia viwanja vya ndege na wageni 4,644 walitumia usafiri wa baharini kupitia Bandari ya Malindi Zanzibar.

"Kati ya wageni 45,915 waliofika Zanzibar, 20,203 walikuwa wanaume na 25,712 wanawake. Asilimia 8.9 ni wenye umri kati ya miaka 65 na asilimia 85 ni wenye mri kati ya miaka 15 hadi 64," alibainisha.

Alifafanua kuwa wageni asilimia 99.7 ya wageni hao walitembelea Zanzibar kwa ajili ya mapumziko, asilimia 0.2 walifika kwa lengo la kuwatembelea ndugu na marafiki na asilima 0.1 walikuja kwa sababu nyinginezo na walikaa Zanzibar kwa wastani wa siku 10.

# Athari ukataji miti zaanza kujitokeza Morogoro

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

ATHARI za uharibifu wa mazingira katika maeneo mbalimbali ikiwamo vyanzo vya maji zinazochangiwa na ukataji wa miti, uchomaji mkaa na shughuli za kibinadamu kwenye hifadhi za misitu Mkoa wa Morogoro zimeanza kujitokeza kwa baadhi ya maeneo kutokana na kukosekana kwa mvua ya masika inayoendelea kunyesha kwenye maeneo mbalimbali ya nchi.

Serikali ya mkoa huo imeonya kuwachukulia hatua kali watakaobainika kuchezea na kufanya shughuli za kibinadamu katika vyanzo vya maji katika mito inayotiririsha maji kwaajili ya wakazi zaidi milioni 11 wanaotegemea mito hiyo na katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

Agizo hilo,limetolewa na Katibu Tawala Msaidizi upande wa Uchumi na Uzalishaji , Dk Rozalia Rwegasira, wakati wa ugawaji wa miche ya karafuu na mazao ya viungo kwa wakulima wanaolima kandokando ya mito pamoja na vyanzo maji kwenye mito tegemezi katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.

Dk. Rozalia alisema, hatua ya serikali ya mkoa huo kupiga marufuku inatokana na vyanzo vya maji ikiwamo chemichemi zinazopeleka maji kwenye mito kuharibiwa na shughuli za kibinadamu ikiwamo kilimo, kuchoma mkaa na kukata kuni.

Alisema kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro kwa kushirikiana na Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani(WWF), limeanza mkakati maalumu wa uhifadhi wa mazingira katika vyanzo vya maji kwenye mito tegemezi inayopeleka kwa wakazi zaidi milioni 11 wa mikoa ya Pwani, Dar es Salaam na Morogoro.

Ofisa Programu wa Maendeleo Endelevu Afrika wa WWF, Happness Minja, alisema katika kutekeleza mpango huo wameamua kutoa bure miche 20,000 ya miti ya karafuu kwa wakulima wanaolima kandokando ya mito hiyo pamoja na vyanzo maji ili waweze kupanda na kisha kujinufaisha kiuchumi huku wakiendelea kutunza vyanzo hivyo.

Alisema mpango huo utahusisha maeneo ya vyanzo vya chemichemi hai zinazotiririsha maji na kujaza vijito na mito yatapandwa miti rafiki ya matunda na karafuu na mazao ya viungo ambayo inasaidia kutunza na kuhifadhi mazingira kwenye maeneo ya vyanzo vya maji.

Minja, alisema mradi huo utahusisha kata nne zinazopitiwa na mito hiyo muhimu kwaajili ya vyanzo vya maji.

Alisema lengo kuu la mradi huo pamoja na utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji pia kukuza uchumi wa wakulima kupitia upandaji wa miti ya mazao ya viungo na matunda.

Alitaja maeneo yatakayopandwa miti hiyo ni Mto Mbezi, Kijiji cha Bagilo, Kata ya Tegetero, wananchi wanaolima chanzo cha maji cha Mto Mfizigo, Kijiji cha Tandai na Kalundwa, Kata ya Kinole.

Wengine ni wanaolima pembezoni mwa mito katika kijiji cha Kiswira, kata ya Konde na Mto Mtombozi kwa wananchi wa kijiji cha Mtombozi na Lusange, Kata ya Mtombozi, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.

Ofisa Kilimo wa halmashauri ya wilaya hiyo, Chesco Lwaduka, alisema halmashauri hiyo imefanya utafiti inahitaji miche 1,113,042 ya karafuu, mdalasini miche 12,155,578, pilipili manga miche 5,825,212 na iliki miche 5,452,709.

Alilishukuru Shirika la WWF kwa kujitolea miti ya viungo.

Mkuu wa kidakio cha Ruvu Kati kutoka Ofisi ya Bonde la Wami/Ruvu, Richard Mwasenga, alisema faida ya kupanda miti hiyo pembezoni mwa vyanzo vya maji ni kusaidia kingo za mito na mmomonyoko wa ardhi.




Mwenyekiti wa umoja wa wanafunzi waliowahi kusoma katika shule ya vipaji maalumu ya Sekondari ya Mzumbe (Alumni), mkoani Morogoro, Edward Tarawa (wa tatu kulia), akikabidhi moja ya vitabu zaidi ya 4000 vya kiada na ziada kwa Mkuu wa shule hiyo, Mbaraka Mohamed, shuleni hapo wilayani Mvomero hivi karibuni. Wengine ni Mkuu wa mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye (kulia) na (kushoto) ni Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa shule hiyo, Donald Tarawa. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Masomo ya dini kutiliwa mkazo shuleni

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

ILI kukabiliana na vitendo vya mmomonyoko wa maadili kwa jamii, serikali imeombwa kutilia mkazo masomo ya dini shuleni ili kumaliza hali hiyo hususani kwa vijana.

Mkurugenzi wa Mungu Anaweza Mission International, Kibaha, Paul Philipo alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kukabiliana na vitendo hivyo.

Alisema, masomo hayo yanapaswa kutiliwa mkazo ili iwe sehemu ya kuwafundisha wanafunzi kumheshimu Mungu na kuwatahadharisha vitendo viovu.

Philipo alisema kuna haja ya kuzungumzia mambo yanayohusu vitendo vya ushoga ambavyo kwa sasa ni tatizo la kidunia na masuala mengine ambayo yanashamiri katika mmomonyoko wa maadili.

Pia, alisema dunia imeathirika, lakini Taifa la Tanzania Mungu amelibariki na wao wataendelea kuwafundisha vijana wapate neno la Mungu likae ndani ya vijana na jamii.

Alisema kwasasa wanaendelea kuliombea taifa na vijana kwa ujumla ili kupunguza athari kwa jamii hususani kwa watoto ambao bado wako shule.

Mkoa wa Pwani ni kati ya maeneo mengine ambayo wapo wazazi wanaoripotiwa kuwafanyiwa vitendo vya ukatili watoto wao jambo ambalo ni kinyume na maadili ya Kitanzania.

# Wananchi Maswa watakiwa kupisha mradi umeme

**Na Alex Sayi,** MASWA

SERIKALI wilayani Maswa mkoani Simiyu imewataka wakazi wilayani humo wanaopitiwa na mradi wa umeme wenye msongo wa kilovoti 220, ukitokea Itabadakuli mkoani Shinyanga hadi Bariadi Simiyu, kuachia maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ili uweze kukamilika kwa wakati.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Aswege Kaminyoge, wakati akizungumza na watendaji wa vijiji, kata pamoja na baadhi ya wamiliki wa maeneo hayo na kueleza kuwa watalipwa stahiki zao mapema iwezekanavyo.

Alisema mradi huo utatekelezwa ndani ya miaka miwili kuanzia Aprili 18, mwaka huu na utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 48.7 na kuwaomba kuruhusu shughuli za awali za mradi huo kuendelea licha ya kuwa bado hawajalipwa fidia zao.

"Ninawaomba mniamini mruhusu shughuli za awali za utekelezaji wa mradi huu ziendelee na kuna wataalamu watapita kwenye maeneo yenu kuchukua sampuli za udongo kupeleka maabara najua bado hamjalipwa ila ndani ya miezi miwili mtakuwa mmelipwa stahiki zenu," alisema Kaminyoge.

Elen Nyanza, mkazi wa Malita alisema, kinachoendelea kwa sasa ni kinyume na makubaliano ya mkataba waliouingia kuhusu utekelezaji wa mradi huo uliokuwa ukionyesha kulipwa ndani ya miezi sita, lakini sasa imepita miezi minane hawajalipwa stahiki zao.

"Mpaka sasa tayari makubaliano ya mkataba yamekiukwa na bado tunaambiwa tupishe maeneo, mradi unaanza na sisi tunalipwa baada ya miezi miwili hii sio haki maana ni kama mnatulazimisha kutoa maeneo yetu," alisema Nyanza.

Mkuu wa Idara ya Ardhi, wilayani Maswa, Viviani Mkamba, alisema wakazi 434 wanaoishi kwenye vijiji 15 vinavyopitiwa na mradi huo, wanatarajiwa kulipwa fidia ya maeneo yao na uhakiki unaendelea.

"Ni wakazi wa vijiji vya Malita, Zanzui, Mwashegeshi, G'hami, Mwabomba, Mondo, Hinduki, Mwang'huhi, Matalambuli, Chuli, Busamuda, Isulilo, Njiapanda na Wigelekelo watakaolipwa fidia ya maeneo yao," alisema Vivian.

**Wakazi 434 wanaoishi kwenye vijiji 15 vinavyopitiwa na mradi huo, wanatarajiwa kulipwa fidia ya maeneo yao na uhakiki unaendelea.**

## HABARI KIMATAIFA

# Miili 21 yapatikana kanisa tata Kenya

**NAIROBI,** Kenya

MIILI 21 ya waumini wa Kanisa la Good News International Church linaloongozwa na mchungaji Paul Mackenzie, ambaye amekuwa akichunguzwa na polisi kwa madai ya kuwataka waumini wake kufa njaa ili kufika mbinguni kwa haraka imegundulika katika eneo la Kilifi, nchini Kenya.

Taarifa ya polisi ilisema idadi hiyo ilipatikana huku msako wa maofisa wa ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka ya Umma (DCI), ukiingia siku ya tatu.

**Wengi wanajiuliza maswali mengi kuhusu mazingira yaliyosababisha kufa kwa njaa kwa waumini wa kanisa hilo.**

Pia inaelezwa kwamba miili hiyo ilipatikana Jumamosi baada ya maofisa wa DCI kuchimba makaburi mafupi yaliyokuwa kwenye kipande cha ardhi katika kijiji cha Shakahola Kaunti ya Kilifi.

Inadaiwa kuwa kiongozi wa kanisa hilo Paul Mackenzie, aliwalazimisha waumini wake kuanzia watoto wadogo hadi watu wazima kufunga kula chakula hadi kufa kama njia ya moja kwa moja ya kufika kwa muumba wao.

Inadaiwa kuwa Mackenzie, ambaye kwa sasa yuko katika mahabusu ya polisi, wakati uchunguzi dhidi yake ukiendelea, amefanya mgomo wa chakula.

Pia inaelezwa kuwa wengi wanajiuliza maswali mengi kuhusu mazingira yaliyosababisha kufa kwa njaa kwa waumini wa kanisa hilo.

Aidha, inaelezwa kuwa mashirika ya kutetea haki za binadamu kwa sasa yanawashutumu maofisa wa Malindi kwa kushindwa kuchukua hatua baada ya kupata taarifa za ujasusi ambazo zingezuia mafundisho ya itikadi kali ya mchungaji Paul Makenzie kwa muda unaofaa.

Mashirika ya haki za kibinadamu yanaitaka serikali kuchukulia kwa uzito suala hilo kulingana na uzito wake, na kuwawajibisha waliozembea kuchukua hatua za kudhibiti vifo vya waumini wa kanisa hilo. **BBC**

# Muswada kuundwa jeshi la akiba wakolea DRC

**KINSHASA,** DRC

WABUNGE nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wamejadili muswada wa kuundwa kwa jeshi la akiba, kwa lengo la kupambana na uvunjifu wa usalama, mashariki mwa nchi hiyo.

Waziri wa Utafiti wa Kisayansi ambaye pia ni waziri wa zamani wa ulinzi, Gilbert Kabanda, alisema muswada huu unalenga kuunda askari wa akiba ambao wanaweza kutoa msaada wa kijeshi wakati wanapohitajika kufanya hivyo haswa wakati huu ambapo DRC inakabiliwa na changamoto za kiusalama katika eneo la mashariki.

"Ili kukomesha uchokozi wa mara kwa mara ambao nchi inakabiliwa nao na kuimarisha zaidi ulinzi wa mamlaka yake na uadilifu wa eneo lake, kuundwa kwa jeshi la akiba ya ulinzi ni muhimu, hii itakuwa na sifa ya kudumisha moyo wa kulinda nchi na kuimarisha uhusiano kati ya taifa na wananchi wake," alisema Kabanda.

Spika wa Bunge la DRC Christophe Mboso, alisema kutokana na utaratibu wa dharura serikali iliomba bunge kujadili suala hilo kwani DRC ni nchi ambayo haiko kwenye orodha za nchi ambazo zina jeshi la akiba.

Aidha, inaelezwa kuwa licha ya wabunge wa upinzani kukosoa muswada huo, baada ya majadiliano wote walikubaliana kuwa muswada huo upitishwe kama alivyopendekeza naibu spika wa bunge la DRC Andre Mbata.

"Baada ya mjadala na upigaji kura matokeo yako hivi, wabunge 384 walishiriki kikao na wote walikubali muswada huu upitishwe," alisema Mbata.

DRC ambayo ina kikosi cha wanajeshi 150,000, sasa imepanga kupeleka muswada huo kwenye bunge la seneti kwa ajili ya kujadiliwa kwa mara ya pili.

Hatua hiyo ya bunge pia inakuja wakati huu wanajeshi wa jumuiya ya Afrika Mashariki wakiwa nchini DRC kusaidiana na wanajeshi wa nchi hiyo katika kuimarisha usalama. **RFI**





Kushoto ni kiongozi na Mkuu wa Jeshi la Sudan, Abdul Fattah Al-Burhan na kiongozi wa kikosi cha RSF Mohamed Hamdan Dagalo, wakuu wa kijeshi nchini Sudan ambao vikosi vyao vinaendelea kukabiliana.

# Raia wa kigeni waondolewa Sudan

**KHARTOUM,** Sudan



Raia wakikimbia mapigano. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

KIONGOZI wa Sudan ambaye pia ni mkuu wa jeshi, Abdel Fattah al- Burhan, ameridhia kuhamishwa raia na wawakilishi wa kidiplomasia kutoka katika nchi hiyo ambayo imekuwa kwenye mapigano kwa wiki ya pili sasa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na msemaji wa jeshi la Sudan, alisema Marekani, Uingereza, Ufaransa na China zitaanza shughuli za kuwahamisha raia wake kutoka kwenye mji mkuu wa Sudan, Khartoum muda usio mrefu kwa kutumia ndege za kijeshi.

Jeshi limesema mkuu wake, Jenerali Abdel Fattah Burhan, alizungumza na viongozi wa nchi kadhaa ambao wameomba raia na wanadiplomasia wao kuondolewa salama kutoka nchini Sudan.

Al-Burhan aliahidi kuwezesha na kudhamini zoezi la kuwahamisha watu na kuzipa nchi hizo msaada unaohitajika ili kuhakikisha zoezi hilo linafanikiwa.

Msemaji wa jeshi alieleza kwamba wajumbe wa Saudi Arabia tayari wameondolewa kutoka kwenye mji wa mashariki wa Port Sudan, na kwamba wajumbe wa Jordan pia wanatarajiwa kusafirishwa kwa ndege kutoka Port Sudan.

Pia Jordan ilisema inafuatilia kwa karibu hali ya usalama ya nchini Sudan na kwamba inashirikiana na Saudi Arabia na nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu.

Wizara ya ulinzi ya Marekani wiki iliyopita ilisema itawapeleka askari wa ziada na vifaa katika kituo cha wanamaji kilichopo Djibouti kwa ajili ya kujiandaa kwa zoezi la kuwaondoa wafanyakazi wa ubalozi wa Marekani.

Wakati huo huo ikulu ya Marekani hadi Ijumaa ilisema serikali haikuwa bado na mpango wa kuratibu zoezi la kuwahamisha takriban raia 16,000 wa Marekani ambao wamekwama nchini Sudan.

Aidha, inaelezwa kuwa ingawa pande zinazopigana zilikubaliana kusitisha mapigano kwa siku tatu ili kutoa nafasi ya kuadhimisha Sikukuu ya Eid el-Fitr, milipuko na milio ya risasi iliendelea kusikika kote katika jiji la Khartoum Jumamosi.

Mara mbili makubaliano ya kusitisha mapigano yaliyofikiwa mapema wiki hii yalikiukwa ndani ya muda mfupi pia.

Katibu wa muungano wa madaktari wa Sudan, unaofuatilia na kuratibu watu waliojeruhiwa Atiya Abdalla Atiya, alisema watu wanapaswa kutambua kuwa vita vimekuwa vikiendelea tangu siku ya kwanza vilipoanza.

Kulingana na ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO), mapigano hayo yamesababisha vifo vya watu zaidi ya 400 kufikia jana, na kwamba watu wengine 3,551 wamejeruhiwa kwenye mgogoro huo.

Mkuu wa jeshi la Sudan Jenerali Abdel Fattah al-Burhan aliambia televisheni ya Al Arabiya kwamba pande zinazopigana zinahitaji kukaa chini na kuzungumza kama Wasudan ili kutafuta njia sahihi ya kurejesha matumaini na hali ya maisha ya kawaida kwa watu wa Sudan. **DW-AP/RTRE**

## HABARI MICHEZO

# MIAMBA YA 'LIGI KUU' KUFUNGUA MTIFUANO LIGI DARAJA LA PILI LEO

**Na Adam Fungamwango**

TIMU zilizowahi kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara, Stand United na Alliance FC, leo zitapambana kwenye ufunguzi wa Ligi Daraja la Pili nchini kusaka timu tatu zitakazocheza Ligi ya Championship msimu ujao.

Mechi hiyo itacheza kwenye Uwanja wa Azam Complex, ambapo michuano hiyo itapigwa ikizikutanisha timu nane ambazo zimepangwa kwenye makundi mawili.

Stand United iliteremka daraja msimu wa 2018/19, huku Alliance FC ikishuka msimu wa 2020/21.

**Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara mwaka 1967, Cosmopolitan, wao wataingia dimbani, saa 1:00 usiku kucheza dhidi ya Lipuli FC, timu nyingine iliyowahi kucheza Ligi Kuu.**

Ligi hiyo itaendelea kesho wakati African Lyon nayo itacheza na wenzao ambao walikuwa Ligi Kuu msimu wa 2013/14, Rhino Rangers jioni, kabla ya TMA na Dar City kukipiga usiku.

Timu hizo zimepangwa kwenye makundi mawili, A na B, ambapo Stand United, Allinace FC, Cosmopolitan na Lipuli zipo kundi A na African Lyon, Rhino Rangers, TMA na Dar City zipo Kundi B na zitakipiga hadi Mei 2, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Mpiga wa Miguu nchini (TFF), nusu fainali zote mbili zinatarajiwa kuchezwa Mei Mosi na fainali itachezwa Mei 3, mwaka huu pamoja na mechi ya kusaka mshindi wa tatu.

Taarifa inasema kuwa timu zitakazocheza fainali zote zitakuwa zimeshapanda Ligi ya Championship, ambapo timu zitakazofungwa kwenye hatua ya nusu fainali nazo zitacheza mechi ya kusaka mshindi wa tatu ambaye ataungana na timu mbili zilizotinga fainali kupanda kwenye ligi hiyo.




Mshambuliaji wa Wydad Casablanca ya Morocco, Hamid Ahadad, akijaribu kumzuia kiungo mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama, katika mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na wenyeji kuibuka na ushindi wa bao 1-0. Kushoto ni Sadio Kanoute. **MPIGAPICHA WETU**

## Plujim kuianzia kazi Yanga leo

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van Pluijm, leo anaanza mikakati ya kuivaa Yanga, Mei 4, mwaka huu, kwa kukipa kikosi chake mazoezi maalum baada ya kurejea nchini akitokea Marekani.

Pluijm (pichani) alikwenda nchini Marekani kwa mapumziko mafupi kutokana na matatizo ya kifamilia ambapo amerejea wiki iliyopita tayari kujiandaa na mechi zilizobakia za Ligi Kuu Bara na FA ambapo leo Jumatatu ndio anaanza programu zake maalum alizoziandaa.

Singida Big Stars ina michezo miwili dhidi ya Yanga wakianza na mechi ya Ligi Kuu Bara Mei 4 kisha watashuka tena dimbani Mei 7, mwaka huu kucheza mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA utakaopigwa Uwanja wa Liti mjini Singida.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Singida Big Stars, Hussein Massanza, alisema Pluijm na benchi lake la ufundi leo watakuwa na programu maalum ikiwa ni maandalizi ya mchezo dhidi ya Yanga.



"Kikosi chetu kilipumzika wiki moja baada ya mchezo wetu dhidi ya Polisi Tanzania, baada ya hapo tuliendelea na mazoe bila ya makocha wetu Hans ambaye alikwenda Marekani kwa mambo binafsi ya kifamilia pamoja na Msaidizi wake, Mathias [Lule], ambaye alifiwa na mama yake mzazi, laki sasa wote wamelejea kuendelea na kazi.

"Makocha wote wataendelea na programu zao kama kawaida, Jumatatu ya tarehe 24 [leo]ikiwa ni pamoja na majukumu yao na watakuwa na programu maalum kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wetu wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Yanga.

"Hali ya kikosi kipo vizuri wachezaji wote wana morali ya hali ya juu kuhakikisha tunafanya vizuri katika michezo yetu iliyobakia kabla ya msimu kumalizika," alisema Massanza.

# *JKT Tanzania yarejea Ligi Kuu kwa kipigo*

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuchapwa mabao 3-2 dhidi ya Kitayosce juzi kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora, timu ya JKT Tanzania imerejea Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya misimu miwili kupita.

Timu hiyo iliyoshuka msimu wa 2020/21, itacheza tena Ligi Kuu msimu ujao wa 2023/24, licha ya kipigo hicho kwenye Ligi ya Championship, na kubakisha mechi mbili.

JKT Tanzania imepanda kutokana na matokeo ya mechi ya Pamba ambayo juzi ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbuni kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Kwa matokeo hayo, pointi 62 ilizonazo zinaweza kufikiwa na Kitayosce tu kama watashinda mechi zote tatu walizosaliwa nazo, huku Pamba kama itashinda zote itafikisha pointi 61 tu.

Ni timu mbili tu ambazo zinatakiwa kupamba moja kwa moja Ligi Kuu Tanzania Bara, huku mbili zingine zikisubiri hatma yao kwenye mechi za mchujo.

Kitayosce imefanikiwa kutoka na ushindi huo kwa 'hat-trick' ya Moses Nassor dakika ya 31, 44 na 88 iliyoifanya kuwa kwenye nafasi ya pili kwa pointi 53 ikibakisha mechi tatu, huku Pamba baada ya sare ya juzi ikiwa nafasi ya tatu kwa pointi 52.

Baada ya JKT Tanzania kupamba, Kitayosce na Pamba ndizo zinazoonekana kupigana vikumbo kuitafuta nafasi moja ya kupanda moja kwa moja zote zikiwa zimecheza mechi 25 na kubakisha mechi nane.

Kwa maana hiyo hakuna timu yoyote inayotakiwa kupoteza, huku kila moja ikimuombea mwenzake mabaya.

Mechi zingine za Championship zilizochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Transit Camp ilishinda bao 1-0 dhidi ya Mbeya Kwanza na Fountaine Gate ililazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani, CCM Gairo, Morogoro dhidi ya Mashujaa.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### OSIMHEN ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imeonesha nia ya kumsaka Victor Osimhen, 24, baada ya kutuma ujumbe wa kumfuatilia mshambuliaji huyo Mnigeria anayeichezea Klabu ya Napoli. ***(Star)***

#### POSTECOGLOU AFIKIRIWA

KOCHA wa Celtic, Ange Postecoglou, ni mmoja anayefikiriwa miongoni mwa watu watakaochukua kazi ya ukocha Chelsea, ingawa kocha wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino, amebaki kuwa ndiye mgombea mkuu wa kazi hii. ***(Guardian)***

#### MESSI KUACHIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain itamuacha Lionel Messi aondoke kwa uhamisho huru wakati mkataba wake utakapoisha msimu huu huku klabu hiyo ikipanga hali yake ijayo ya kudumu zaidi kwa majina machache ya wachezaji nyota na kutilia mkazo zaidi katika kuendeleza vipaji vya vijana. ***(Mirror)***

#### NAGELSMANN AITAKA SPURS

JULIAN Nagelsmann, ambaye alijiondoa katika kinyang'anyiro cha ukocha kule Chelsea wiki iliyopita, ana nia ya kujiunga na Tottenham Hotspur. ***(Bild)***

#### RAPHINHA NA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inapanga kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Mbrazili Raphinha, 26. ***(Mundo Deportivo)***

#### ALLISTER KWA LIVER, UNITED

MANCHESTER United na Liverpool zina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Argentina, Alexis Mac Allister, 24, kutoka Klabu ya Brighton. ***(Fabrizio Romano)***

#### WALKER ATAJWA VILLA

KLABU ya Aston Villa inaangalia uwezekano wa kulipa dau mara dufu la pauni milioni 53 kwa ajili ya mlinzi wa Manchester City, Kyle Walker, 32 na kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips, 27. ***(Football Insider)***

#### WATKINS MKATABA MPYA

MCHEZAJI Ollie Watkins, 27, amekubali mkataba mpya wa muda mrefu pele Aston Villa licha ya klabu kama vile Arsenal, Tottenham Hotspur na Newcastle United kuelezea nia ya kumsaka. ***(Teamtalk)***

#### FERNS AKARIBIA BRIGHTON

KLABU ya Brighton inakaribia kumsajili mlinzi mzaliwa wa Scotland, Ronan Ferns, 16, kutoka Klabu ya Celtic. ***(Football Insider)***


#### 10 KUBAKI CHELSEA

TAKRIBAN wachezaji 10 wa Chelsea wanatarajiwa kuendelea kubaki katika klabu hiyo kwa siku zijazo baada ya kushindwa kwao katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na Real Madrid wiki iliyopita. ***(Standard)***

#### MOREIRA SAFI CHELSEA

CHELSEA imekubali kusaini mkataba mpya na na winga Mreno Diego Moreira, 16, kwa mkataba huru wakati mkataba wake na Benfica utakapomalizika msimu ujao. ***(Record)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# COURTOIS: REAL MADRID HAKUNA KUKATA TAMAA

**MADRID,** Hispania

GOLIKIPA Thibaut Courtois amesisitiza kwamba, Real Madrid haijakata tamaa ya kuwafikia vinara wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Barcelona kwenye mbio za ubingwa.

**Ingawa Madrid ilishinda mabao 2-0 Jumamosi dhidi ya Celta Vigo na kupunguza uongozi wa Barcelona hadi pointi nane, Wakatalunya hao jana Jumapili walikuwa na mchezo wa nyumbani dhidi ya Atletico Madrid.**

Iwapo Barcelona walishinda mchezo huo, uongozi wao unarejea hadi pointi 11 huku zikiwa zimesalia mechi nane Ligi kumalizika.

Hata kama Barcelona walipoteza, uongozi wao bado unaendelea na kuwa na nafasi kubwa ya kulitwaa taji hilo.

> ●●● Tutapambana hadi mchezo wa mwisho, mpaka ionekane hesabu haziwezekani...

Bado, Madrid hawaoni sababu ya kukata tamaa, huku kipa Courtois akikiambia Kituo cha Televisheni cha DAZN: "Tutapambana hadi mchezo wa mwisho, mpaka ionekane hesabu haziwezekani."

Alisema "inasikitisha" Madrid walipoteza pointi wakati fulani msimu huu, lakini akaashiria kwamba Ligi ya Mabingwa Ulaya iliathiri matokeo ya nyumbani.

Madrid wamefuzu nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara nyingine tena msimu huu, huku mechi za nyumbani na ugenini dhidi ya Manchester City zikipigwa Mei, pamoja na fainali ya Copa del Rey dhidi ya Osasuna.

Mchuano huo wa kombe unakuja Mei 6, na Courtois alisema: "Tunataka kushinda katika siku tatu za mechi zijazo na wakati wa fainali ya kombe ukifika, tutaona jinsi tuko mbali.

"Tunataka kuendelea kushinda na kuwa na hisia nzuri mbele ya Ligi ya Mabingwa. Ni muhimu kwamba sote tuko vizuri. Tunatumaini tutamaliza msimu vema."

Kocha Mkuu wa Madrid, Carlo Ancelotti, alifanya mabadiliko matano kwenye kikosi chake cha kwanza, siku nne baada ya timu yake kushinda mabao 2-0 dhidi ya Chelsea na kupata ushindi wa jumla wa 4-0 wa robo fainali dhidi ya klabu yake ya zamani kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 560,

MECHI KALI
GEITA GOLD FC
VERSUS
TANZANIA PRISONS
1 | 1.66
X | 3.35
2 | 5.20

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# TUCHEL: BAYERN MUNICH IMECHOKA

**MUNICH,** Ujerumani

THOMAS Tuchel anadhani Bayern Munich inafanana na "timu ambayo imecheza mechi 70 au 80", baada ya 'Wabavaria' hao kuchapwa mabao 3-1 na Mainz juzi, Jumamosi.

Bayern walionekana kuwa na uwezekano wa kuendeleza uongozi wao juu ya wanaoshika nafasi ya pili Borussia Dortmund hadi pointi tano wakati Sadio Mane alipowaweka mbele, lakini wakajikuta wakichezea kichapo kipindi cha pili.

Mabao kutoka kwa Ludovic Ajorque, Leandro Barreiro na Aaron Martin yalimfanya Tuchel kupoteza kwa mara ya tatu katika mechi saba na hivyo kuzima matumaini ya Bayern ya kutwaa taji la 11 mfululizo la ligi msimu huu.


Bayern sasa wamecheza michezo minne bila ushindi katika mashindano yote, na Tuchel anaamini ukosefu wa nguvu ndio uliosababisha kudorora kwao.

"Sidhani ni tatizo la kiufundi au la kimbinu," alisema Tuchel. "Tunaonekana kama tuna miguu iliyochoka, sisi ni wapya. Unahisi kama tunacheza katika muda wa ziada kila tunapoingia uwanjani.

"Ni vigumu sana kuleta matumaini mapya au mawazo mapya, kwa sababu kila mtu anapigana mwenyewe hivi sasa.

"Kuna awamu ndefu katika michezo yote ambapo sisi ni wazuri, halafu katika awamu fupi ambapo hatuko. Tunaacha pointi zipite kwenye vidole vyetu. Inapita mikononi mwetu kama mchanga.

"Hatuna nguvu. Tunaonekana kama timu ambayo imecheza michezo 70 au 80 msimu huu. Tunakosa utimamu wa mwili, nguvu na msingi ambao unahitaji kila wakati."



# Klopp aikatia tamaa Liver

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL "haina chochote cha kufanya" katika mbio za nne bora kwenye Ligi Kuu England kwa wakati huu, kwa mujibu wa Kocha, Jurgen Klopp.

'Wekundu' hao waliifunga Nottingham Forest mabao 3-2 kwenye Uwanja wa Anfield katika mchezo wa kusisimua Jumamosi na sasa wamepitwa pointi sita na Newcastle United iliyopo nafasi ya nne, ingawa wamecheza mechi moja zaidi.

Licha ya kuonesha dalili za ushindi mfululizo wiki hii dhidi ya Forest na Leeds United, Klopp haamini kwamba anaweza kumaliza katika nafasi ya kukata tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa sasa.

"Kusema kweli, nne bora kwa sasa, hatuna chochote cha kufanya," alisema akiiambia BBC Sport.

"Tutaona kuhusu hilo baada ya wiki chache zilizobaki na hatua gani ambazo tutachukua.

"Tunachukulia mchezo kwa mchezo na tuna mechi dhidi ya West Ham ambayo ni ngumu sa
kisha tunatoka hap
Nina furaha tumepa
pointi zote tatu tena."

Liverpool watakuw
na mchezo dhidi ya We
Ham Jumatano kw
mechi tatu mfululiz
za nyumbani, na kut
fursa ya kujenga kasi a
bayo wamekosa msim
mzima.

Bao la Mohamed Sala
la dakika ya 70 lilihi
misha ushindi dhidi y
Forest baada ya Ne
Williams na Morga
Gibbs-White wote k
sawazisha mabao ya D
ogo Jota.

,305,280

JACKPOT

Lorem ipsum

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/04/23 | 21:30 | Wolverhampton vs Crystal Palace | 2.20 | 3.15 | 3.15 |
| 02. 25/04/23 | 21:45 | Lincoln vs Burton | 2.21 | 3.37 | 3.16 |
| 03. 25/04/23 | 22:00 | Leeds vs Leicester | 2.20 | 3.49 | 3.09 |
| 04. 26/04/23 | 01:30 | CA Tigre vs Huracan | 2.36 | 3.01 | 2.91 |
| 05. 26/04/23 | 13:00 | Gangwon vs FC Seoul | 2.53 | 2.93 | 2.67 |
| 06. 26/04/23 | 13:00 | Gwangju vs Jeju Utd | 2.72 | 3.03 | 2.42 |
| 07. 26/04/23 | 13:30 | Suwon City vs Daegu | 2.48 | 3.18 | 2.54 |
| 08. 26/04/23 | 18:30 | Hradec Kralove vs Slovan Liberec | 2.27 | 3.05 | 3.21 |
| 09. 26/04/23 | 21:30 | Servette Geneva vs FC Zurich | 2.31 | 3.26 | 2.89 |
| 10. 26/04/23 | 22:00 | Sheffield Utd vs West Bromwich | 2.21 | 3.24 | 3.29 |
| 11. 27/04/23 | 21:45 | Southampton vs Bournemouth | 2.26 | 3.25 | 2.95 |
| 12. 27/04/23 | 22:00 | Rotherham vs Cardiff | 2.80 | 2.80 | 2.65 |
| 13. 27/04/23 | 22:15 | Tottenham vs Manchester Utd | 2.59 | 3.27 | 2.51 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA

"X" - NI TIMU KUTOKA SARE

"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 24/04/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4499 | SC Dnipro 1 vs Rukh Vinnyky | 1.34 | 4.41 | 7.18 |
| 15:00 | 4862 | Oleksandria vs FC Ingulets | 1.73 | 3.40 | 4.22 |
| 15:30 | 4213 | Aluminium Arak vs Zob Ahan | 2.07 | 2.58 | 4.35 |
| 15:55 | 5960 | AL Ain vs AL Riyadh | 3.49 | 2.93 | 2.07 |
| 16:00 | 1238 | Manisa BBSK vs Altinordu | 1.66 | 3.58 | 4.40 |
| 16:00 | 2533 | Bandirmaspor vs Erzurum BB | 1.80 | 3.44 | 3.80 |
| 16:00 | 3629 | MES Rafsanjan vs Sanat Mes Kerman FC | 1.53 | 3.32 | 6.84 |
| 16:00 | 4322 | Geita Gold FC vs Tanzania Prisons | 1.66 | 3.35 | 5.20 |
| 17:00 | 1116 | AL Khaleej Khor Fakkan vs AL Wahda Scc (UAE) | 4.63 | 3.81 | 1.58 |
| 17:00 | 4072 | Nasaf Qarshi vs FC Olimpik | 1.47 | 3.87 | 5.77 |
| 17:00 | 4421 | Sigma Olomouc B vs Pribram | 2.87 | 3.13 | 2.26 |
| 17:00 | 4680 | Giresunspor vs Basaksehir | 2.78 | 3.30 | 2.37 |
| 17:00 | 5326 | Ajman Club vs Al Dhafra | 1.38 | 4.44 | 6.19 |
| 18:00 | 3041 | Haka vs Honka | 2.97 | 3.03 | 2.26 |
| 18:00 | 3452 | Sepahan Esfahan vs Malavan Bandar Anzali | 1.32 | 4.25 | 9.53 |
| 18:00 | 3597 | FK Panevezys vs Banga Gargzdai | 1.26 | 4.85 | 9.09 |
| 18:00 | 3996 | NK Jarun Zagreb vs Kustosija | 2.08 | 3.18 | 3.18 |
| 18:30 | 4682 | Klubi 04 vs FC Futura | 1.18 | 6.64 | 9.55 |
| 18:50 | 1193 | AL Arabi vs Al Salmiyah | 1.62 | 3.65 | 4.00 |
| 19:00 | 3516 | ZKS Stal Rzeszow vs Sandecja | 2.05 | 3.29 | 3.13 |
| 19:00 | 3931 | Spartak Moscow vs FC Krasnodar | 1.89 | 3.61 | 3.51 |
| 19:00 | 4120 | Karmiotissa vs Akritas Chlorakas | 1.81 | 3.65 | 3.96 |
| 19:00 | 4350 | Borac Banja Luka vs FK Igman Konjic | 1.35 | 4.23 | 8.05 |
| 19:00 | 4531 | Foolad Khuzestan vs Naft Masjed Soleyman FC | 1.42 | 3.83 | 7.46 |
| 19:00 | 5761 | Flora II vs Paide Linnameeskond | 1.58 | 4.69 | 4.48 |
| 19:45 | 1566 | Jazira Abu Dhabi vs AL Bataeh (UAE) | 1.27 | 5.33 | 7.38 |
| 19:45 | 3525 | Dibba Al Fujairah vs Al Nasr Dubai | 3.23 | 3.33 | 2.00 |
| 20:00 | 1002 | Ostersunds vs Skovde Aik | 1.95 | 3.46 | 3.73 |
| 20:00 | 1346 | Covilha vs Mafra | 3.08 | 3.18 | 2.19 |
| 20:00 | 1656 | Radomiak Radom vs Lech Poznan | 3.33 | 3.33 | 1.96 |
| 20:00 | 1824 | Brommapojkarna vs Mjallby | 3.07 | 3.17 | 2.13 |
| 20:00 | 1857 | Mjondalen vs Fredrikstad | 2.57 | 3.29 | 2.40 |
| 20:00 | 1994 | Fenerbahce vs Istanbulspor | 1.23 | 5.88 | 9.87 |
| 20:00 | 2508 | Orgryte IS vs Jonkopings Sodra | 2.26 | 3.30 | 3.09 |
| 20:00 | 3723 | Odense vs Lyngby | 1.97 | 3.49 | 3.54 |
| 20:00 | 4475 | IFK Varnamo vs AIK Football | 3.49 | 3.18 | 1.96 |
| 20:00 | 4782 | Antalyaspor vs Sivasspor | 2.22 | 3.26 | 3.05 |
| 20:00 | 5854 | Benfica Lisbon B vs CD Trofense | 2.08 | 3.39 | 3.13 |
| 20:10 | 1946 | Malmo vs Norrkoping | 1.51 | 3.95 | 5.14 |
| 20:30 | 1231 | Voluntari vs Petrolul Ploiesti | 1.90 | 3.19 | 3.98 |
| 21:00 | 1079 | Jong Utrecht vs Jong Ajax | 2.60 | 3.54 | 2.34 |
| 21:00 | 1525 | Al Nasr Riyadh vs Al Wehda | 1.34 | 4.68 | 7.08 |
| 21:00 | 2979 | Jong PSV vs Maastricht | 1.93 | 3.74 | 3.22 |
| 21:00 | 5783 | MTK Budapest vs Soroksar | 1.42 | 4.30 | 5.73 |
| 21:45 | 1832 | Atalanta vs Roma | 2.25 | 3.15 | 3.05 |
| 21:45 | 3519 | Bordeaux vs Grenoble Foot | 1.68 | 3.50 | 4.80 |
| 22:00 | 2953 | Huesca vs Tenerife | 2.94 | 2.94 | 2.44 |
| 22:00 | 4992 | Luton Town vs Middlesbrough | 2.24 | 3.35 | 2.90 |
| 22:15 | 3871 | Vitoria Guimaraes vs Sporting Lisbon | 5.62 | 4.12 | 1.51 |
| 22:15 | 4536 | Stjarnan vs HK Kopavogs | 1.91 | 3.78 | 3.21 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KIDUKU AWASHUKURU MASHABIKI KICHAPO BONDIA WA GEORGIA

**Na Saada Akida**

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Twaha Kiduku, amewashukuru mashabiki wake kwa kujitokeza kwa wingi katika Ukumbi wa Tanzanite mjini Morogoro juzi, Jumamosi na kumpa sapoti kubwa iliyomwezesha kutetea mkanda wake wa UBO Inter-Continental dhidi ya Iago Kiziria kutoka Georgia.

Katika pambano hilo la raundi 10 uzani wa Super Middle, pia Kiduku ameshinda mkanda mwingine mpya wa Ubingwa PST, ambapo alitangazwa mshindi baada ya majaji wote watatu kumpa pointi zaidi ya mpinzani wake huyo.

**Pambano hilo lilikuwa na upinzani mkali kutoka kwa mabondia wote wawili huku Kiziria akionekana kuwa na nguvu kutokana na kupokea ngumi nyingi lakini hakuna ambayo iliweza kumpeleka chini Kiduku.**

"Niwashukuru mashabiki wangu kwa kuweza kujitokeza kwa wingi leo (juzi), kwa sababu naamini ushindi huu wa kuweza kutetea ubingwa wangu umechangiwa na uwapo wao.

"Kuhusu mpinzani, kiukweli hakuwa wakawaida kwa sababu ana nguvu na alikuwa akitumia maarifa yake kuweza kunipiga lakini nashukuru Mungu nimefanikiwa kutetea ubingwa pamoja na kushinda ubingwa mwingine," alisema Kiduku.

Mapambano mengine yaliyopigwa juzi ni kati ya Juma Choki ambaye alifanikiwa kumchakaza kwa pointi za majaji wawili kwa moja Loren Japhet katika pambano la uzani wa Super Feather ambalo lilipigwa kwa raundi nane.

Ally Ngwando naye alifanikiwa kumchapa kwa pointi Jamal Kunoga katika pambano la Super Feather, lililopigwa kwa raundi nane wakati Pascal Goga akipoteza kwa KO ya raundi ya nne mbele ya Ahmed Pelembela katika pambano la uzani wa Light lililopigwa kwa raundi sita.

Habibu Pengo alipoteza kwa pointi mbele ya Said Mkola katika pambano ambalo Pengo amepigika hadi kumsababishia kutapika ulingoni kabla ya kutangazwa mshindi wa pambano hilo.

Sara Alex na Florah Machela waliambulia sare katika pambano la raundi sita kwenye uzani wa Bantam na Joseph Mchapeni alimchapa Emmanuel Mbogo wakati Abdallah Yoba akipoteza mbele ya George Udongo.

## Robertinho tutaivaa Wydad kivingine kwao

INATOKA UK. 24

kazi kubwa na mlima mrefu wa kuupanda Aprili 28, mwaka huu, nchini Morocco ili tumfunge Wydad nyumbani kwake na kusonga mbele lazima tukapambane kiume ugenini," alisema Mo Dewji.

Alisema anaimani kubwa na Simba kufikia rekodi hiyo ya mwaka 2003 kwa sababu ya kuwa na kikosi imara na wachezaji kumhakikishia kupata matokeo mazuri katika dakika 90 zijazo.

Kocha wa Wydad Casablanca, Juan Carlos, alisema hawakuwa na mchezo mzuri kwa sababu hali ya hewa haikuwa rafiki na Simba kutumia madhaifu kwa nafasi waliyotengeneza.

Alisema mechi ilikuwa na ushindani mkubwa na Simba wametumia vizuri uwanja wa nyumbani kupata matokeo mazuri na wao wameshindwa kutumia nafasi walizotengeneza.

"Kusema ukweli hatukuwa na mchezo mzuri leo [juzi] sababu kubwa ni mvua, uwanja haukuwa rafiki na mliona jinsi gani wachezaji walikuwa wakiteleza sana uwanjani.

"Tumemaliza dakika 90 za Dar es Salaam, tunawakaribisha Simba katika mchezo mwingine nyumbani kwetu Morocco, lazima tupambane tushinde mchezo huo kwa sababu malengo yetu ni kucheza nusu na fainali, ninawapongeza Simba kwa ushindi walioupata," alisema Carlos.



Bondia Twaha Kiduku (kulia), akimrushia makonde mpinzani wake, Iago Kiziria, katika pambano la kuwania mkanda wa UBO Inter-Continental lililofanyika Ukumbi wa Tanzanite mjini Morogoro juzi, Jumamosi. Kiduku alifanikiwa kutetea mkanda huo kwa kushinda kwa pointi dhidi ya bondia huyo raia wa Georgia. **MPIGAPICHA WETU**

## *Yanga SC mguu sawa*

INATOKA UKURASA 24

Nafasi nyingine ya wazi kwa Yanga kukosa ilikuwa ni dakika ya 26, Aziz Ki alipowapangua mabeki wa Rivers United kabla ya kupiga shuti kali lililotemwa na kipa, ukadondoka miguuni mwa Mudathir Yahaya ambaye shuti lake lilipaa juu ya lango.

Kipa Sochima alifanya kazi ya ziada dakika ya 42, alipolazimika kuchupa kudaka mpira wa kichwa uliopigwa na Mudathir, baada ya kuunganisha krosi maridadi ya Farid Mussa.

Kipindi cha pili Kocha Nasreddine Nabi akalazimika kufanya mabadiliko ya mfumo baada ya kuwaona wapinzani wao si hatari kama alivyodhania, akaamua kuachana na kuweka mabeki na viungo wakabaji wengi na kuamua kuweka mawinga na kushambulia.

Akawatoa Djuma Shaaban, Joyce Lomalisa, Farid Mussa na kuwaingia Moloko, Tuisila Kisinda na Kibwana Shomari, mabadiliko ambayo yalisaidia sana kupatikana kwa ushindi huo, huku baadaye pia akiwaingiza Aucho badala ya Yannick Bangala na Mudathir akimpisha Zawadi Mauya.

Endapo Yanga ikipata matokeo ya jumla Jumapili, hatua ya nusu fainali itakutana na timu itakayotinga hatua hiyo kati ya Pyramids ya Misri ama Marumo Gallants FC ya Afrika Kusini, ambazo zilicheza jana usiku.

# Michezo

Jumatatu Aprili 24, 2023

Nipashe




Klopp aikatia tamaa Liverpool UKURASA 22

# Yanga SC mguu sawa nusu fainali Shirikisho

## ●●● Mayele ailowesha Rivers United akipaa kileleni kwa ufungaji, sasa waichukulia...



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akishangilia baada ya kufunga bao lake la pili wakati wakishinda 2-0 dhidi ya Rivers United, kwenye mechi ya mkondo wa kwanza ya robo fainali Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Godswill Akpabio, Nigeria jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara, Yanga, wameingiza mguu mmoja kutinga nusu fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika baada ya kupata ushindi ugenini wa mabao 2-0 dhidi ya Rivers United ya Nigeria, mechi ikipigwa Uwanja wa Godswill Akpabio, kwenye mji wa Uyo nchini humo.

**Yalikuwa ni mabao ya straika raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Fiston Mayele, aliyefunga mabao yote mawili, akifikisha jumla ya mabao matano kwenye michuano hiyo kabla ya mechi zingine kuchezwa jana.**

Alifunga bao moja kwenye mechi dhidi ya Monastir, Yanga ikishinda 2-0 nyumbani, dhidi ya Real Bamako ugenini kwenye sare ya bao 1-1, bao lingine akifunga dhidi ya timu hiyo hiyo katika ushindi wa mabao 2-0 nyumbani.

Katika mchezo wa jana, Mayele alianza kutupia dakika ya 75, baada ya kazi nzuri iliyofanywa na nahodha wa timu hiyo, Bakari Mwamnyeto, aliyepanda mbele kusaidia mashambulizi, akapiga pasi mpenyezo iliyomkuta Mkongomani huyo aliyekuwa amewatoroka mabeki wa Rivers United, kabla ya kubaki na kipa Victor Sochima, akaubetua juu kidogo mpira ukakwama nyavuni.

Dakika sita baadaye, Mayele alipachika bao la pili kirahisi zaidi kutokana na uzembe mkubwa wa wachezaji wa River United.

Faulo iliyopigwa na wachezaji wa timu hiyo, ilimkuta mchezaji Naziru Auwalu ambaye alitaka kupiga shuti, akaukosa na kuanguka mwenyewe, haraka sana, Jesus Moloko aliyeingia kipindi cha pili aliuchukua mpira na kukimbia nao kwa kasi, akampa Khalid Aucho ambaye naye aliingia kipindi cha pili, mpira ukamfikia Mwamnyeto kwa mara nyingine tena akamtengea mfungaji aliyekwamisha wavuni.

Yanga imelipa kisasi cha kufungwa na timu hiyo mara mbili bao 1-0 nyumbani na ugenini msimu uliopita kwenye hatua ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikifungwa nyumbani Septemba 12, mwaka 2021, ikapoteza tena Septemba 19, mwaka huo nchini Nigeria.

Ni ushindi ambao unaonekana kuwarahisishia kazi kwenye mechi ya mkondo wa pili wa robo fainali ya Kombe la Shirikisho, utakaochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Aprili 30, mwaka huu.

Mechi ilianza kwa kila timu kutafuta bao la mapema, na dakika ya pili tu nusura wenyeji wafunge, kutokana na faulo iliyopigwa na Chidiebube Duru, lakini mpira ulipaa juu ya lango.

Baada ya shambulizi hilo, ni kama Yanga ilitiwa funguo kwao ilianza kulishambulia lango la wapinzani wao kama nyuki, dakika ya nane Stephane Aziz Ki akikosa bao, dakika moja baadaye alikaribia kufunga, lakini kipa, Sochima akauwahi.

Dakika ya 15 ya mchezo, Yanga ilikosa bao baada ya mpira wa kona kuleta kizaazaa langoni na katika piga nikupige mpira ulionekana unatinga wavuni, kabla ya beki mmoja wa Rivers United kuufagia kwenye mstari.

Lango la Yanga lilitiwa msukosuko dakika ya 20 kutokana na mpira wa kona uliookolewa kizembe na mabeki, kabla ya kumkuta mchezaji Chukwudi Ekeocha aliyepiga shuti lililoleta tena hatari, lakini wenyeji hawakuwa makini kuutumbukiza mpira ndani ya wavu.

INAENDELEA UKURASA 23

## Robertinho: Tutaivaa Wydad kivingine

**Na Saada Akida**

BAADA ya ushindi hafifu wa bao 1-0 dhidi ya Wydad Casablanca kwenye mechi ya robo fainali ya mkondo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, amesema kazi bado haijamalizika na wataenda na sura mpya katika mchezo wa marudiano utakaopigwa Jumamosi nchini Morocco.

Simba inatarajia kucheza mchezo wa marudiano Aprili 28, mwaka huu, nchini Morocco katika Uwanja wa Mohammed V, kusaka ushindi ama sare yoyote ili kutinga nusu fainali.

Akizungumza na gazeti hili baada ya kukamilika kwa dakika 90 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Robertinho alisema anashukuru na kuwapongeza wachezaji wake kwa kupata matokeo mazuri japo ni ushindi mwembamba.

Alisema hii ni Ligi ya Mabingwa na walikuwa wanacheza na bingwa wa Morocco na mtetezi wa michuano hiyo ya Afrika, hivyo haikuwa kazi nyepesi kuwafunga Wydad.

"Watu wanatakiwa kuipongeza Simba kwa ushindi huu, imeonesha dunia nzima kila mpinzani anatakiwa atuheshimu, tumeonesha tuna ubora mzuri ndani ya uwanja," alisema Robertinho.

Aliongeza kuwa sasa wanarejea katika uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi hiyo kwa ajili ya kujiandaa na kibarua kingine cha mchezo wa marudiano.

Robertinho alisema anatambua itakuwa mechi ngumu na ushindani mkubwa kwa kuwa Wydad watahitaji kutumia vizuri uwanja wao kama ilivyo kwa Simba ikiwa Benjamin Mkapa.

"Haitakuwa mechi rahisi na tutalazimika kucheza kwa mbinu tofauti na mechi ya leo [juzi], na wachezaji kuingia kivingine katika mchezo wa marudiano tofauti na tulivyocheza ili kufikia malengo yetu ya kusonga mbele kucheza nusu fainali," alisema Robertinho.

Alisema kuwa anaimani kubwa na wachezaji aliokuwa nao ndani ya kikosi kwa kufanikisha malengo yao akiwamo Mohammed Hussein [Tshabalala] Saido [Ntibazonkiza], Kapombe [Shomari], Baleke [Jean] na Mzamiru [Yassin] na wengineo.

Rais wa Heshima na Mwekezaji wa Simba, Mohammed 'Mo' Dewji, amewataka wachezaji kwenda kupambana katika mchezo wa marudiano dhidi ya Wydad Casablanca.

"Tunafurahi kwa ushindi huu, lakini bado, tuna

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >